SUPA JACKPOT
TZS.1,093,395,265
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

UKURASA 3



**WASOTA** mwezi gesti kutaka kumwona Waziri Mkuu Majaliwa




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
Jumapili Machi 26, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581261
JUMAPILI
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Kasi watoto kuzaliwa na maradhi yatisha

UKURASA 4



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Othman Masoud Othman, akichagua nazi kutoka katika genge la Mfanyabiashara Ali Khamis Khalfan, katika soko la mboga la Mombasa Mjini Zanzibar, alipofanya ziara kuona mwenendo wa bidhaa na bei mbalimbali katika masoko tofauti kipindi cha mfungo wa Mwenzi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: OMKR.**







## Othman ataka ufumbuzi bei juu za bidhaa mwezi mtukufu

UKURASA 3

## Hiki ndicho kiini cha vijana kutowajibika katika ndoa

UKURASA 2

MICHEZO STARS YAMKOSHA RAIS SAMIA UK. 24
MAONI, KATUNI UK.6

## Maagizo ya RC mgogoro wa ardhi Kigamboni yakwama kwa kamishna

**Na Mwandishi Wetu**

SAKATA la mgogoro wa ardhi kata ya Kimbiji, Manispaa Kigamboni ambao Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alitangaza uamuzi wa serikali wa kuchukua kipande cha ardhi chenye mgogoro, limekwama kwa Kamishna wa Ardhi, imebainika.

Mgogoro huo kati ya kampuni ya ASM (T) Limited na wananchi, ulidumu kwa muda mrefu kabla ya Makalla kuutolea ufumbuzi Desemba 16, mwaka jana, baada ya vikao mbalimbali kufanyika.

Baada ya kufanya ziara mara mbili kwenye eneo lenye mgogoro na kupitia kanuni mbalimbali, Makalla aliagiza Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kuilipa fidia ASM (T) LTD ili ukuta uliojengwa na mwekezaji huyo kufunga barabara inayopita kwenye viwanja vyake 'pacha' ubomolewe kuwezesha wananchi na wawekezaji wengine kwenye eneo la ufukwe kutumia kama barabara kwenda kwenye maeneo yao.

Hata hivyo, uchunguzi wa gazeti ili umebaini suala hilo limekwama kwenye ofisi ya Kamishna wa Ardhi, makao makuu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi licha ya barua ya uamuzi kutumwa kwake tangu Januari, mwaka huu.

Mmoja wa wakazi wa Kimbiji, Abdallah Mbonde, akizungumza na gazeti hili, ,alisema amefuatilia sakata hilo na kubaini kamishna msaidizi wa ardhi mkoa wa Dar es Salaam tayari alishalifanyia kazi na kuandika barua kwa kamishna ili kumjulisha waziri mwenye dhamana kwa ajili ya utekelezaji.

"Tumeshangaa Mkuu wa Mkoa kashatoa maelekezo kwa niaba ya serikali kwenye mkutano Desemba mwaka jana, ambao na mimi nilikuwapo na tumegundua pia barua imeshaandikwa kwa kamishna. Sasa hatujui sababu zinazochelewesha maamuzi ya kulimaliza sakata hili," alisema Mbonde.

Kamishna wa Ardhi, Nathaniel Mathew, alipoulizwa kuhusu suala hilo, alimtaka mwandishi kuwasiliana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika wizara, Anthony Ishengoma, ambaye naye alipotafutwa alisema hawezi kutoa majibu mpaka atakapowasiliana na kamishna.

"Mkuu yuko safarini, sasa siwezi kutoa majibu mpaka niwasiliane naye hivyo naomba usubiri," alisema Ishengoma.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kumwandikia Rais kuomba kutwaa ardhi kwa mmiliki, alisema pamoja na kulifahamu suala hilo, bado barua kutoka kwa Kamishna wa Ardhi haijamfikia mezani kwake.

Kukwama kwa jambo hilo kumeendelea kuwa adha kwa wananchi wa maeneo hayo ambao wengi wao ni wavuvi waliokuwa wakiitumia barabara hiyo kwenda kwenye shughuli zao baharini.

Aidha pia sakata hilo limekuwa kikwazo kwa wawekezaji wa hoteli katika maeneo hayo ambao wamelazimika kufunga hoteli zao kwa kukosa barabara rasmi kuingia kwenye maeneo yao.

Mmoja wa wamiliki wa hoteli katika eneo hilo, Vidate Msoka, alisema wamekwama kwenye biashara zao na kulazimika kuachisha wafanyakazi kutokana na kufungwa kwa hoteli kwa kukosa barabara rasmi.



Mafundi wa kampuni ya Sinohydro wakiendelea na ujenzi wa barabara ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT), Vingunguti, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Hiki ndicho kiini cha vijana kutowajibika katika ndoa

**Na Romana Mallya**

KASI ya vijana hasa wa kiume kutowajibika katika nafasi zao kwenye ndoa imekuwa ikiongezeka kila uchao.

Hatua hiyo imewaibua viongozi wa kidini, kimila na wazazi ambao wamebainisha mambo kadhaa wanayoamini ndicho kiini cha mmomonyoko wa maadili kwa vijana wa kiume, unaochangia kushindwa kwenye nafasi zao katika ndoa.

Baadhi ya mambo yanayotajwa ni pamoja na malezi, mila kusahaulika, kujilea au kulelewa na watu wasio na maadili na wazazi kutumia muda mwingi katika kazi badala ya malezi ya watoto.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwapo kwa janga hilo, vijana wengi wanajiingiza kwenye mapenzi na wanawake umri mkubwa ili kulelewa na wengine kukimbia ndoa.

Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Dk. Charles Kitima, alisema katika makuzi ya mtoto kwenye familia, wazazi wanapaswa kuwa mfano wa kuwawajibisha na kuwafundisha kazi ili wajue kuishi kwa kujitegemea.

"Lakini pia akiwa shuleni, kuanzia shule za msingi zinasisitiza maadili ya kuwajibika na kujua mipaka ya maisha na uhuru. Tukumbuke kufundisha na kutenda inategemea mzazi atafuatilia vipi matendo ya mtoto wake tangu mdogo kuona kama yanaendana na anavyolelewa shuleni.

"Ni wazi kuwa, kwa sasa changamoto kubwa ni hii, wazazi wanakaa na watoto muda gani? Wana muda wa kutosha wa kupima tabia zao? Jibu ni hapana," alisema.

Dk. Kitima alisema usimamizi wa tabia unapaswa kuangaliwa shuleni lakini utengenezaji tabia huko nyuma ulifuatiliwa zaidi na mzazi.

"Watoto walikuwa wanakwenda kufanya shughuli pamoja na wazazi wao kabla haya mambo ya wazazi ya kutokuwa na muda nao kwamba wako 'busy' hayajaanza. Hata shuleni kulikuwa na vipindi vya watoto wanafanya kazi na wanafuatiliwa, wanapewa adhabu wanalima.

"Ukienda nchi nyingine unakuta watoto wamewekwa kwenye makundi mbalimbali kujifunza tabia ya kuwajibika, haya yote ni kuwafanya wajifunze tabia ya uwajibikaji, kujitolea na kujituma na kuonyesha uwezo wa kujitegemea. Hivi sasa mtoto hawajibishwi kuchota maji, kufua hata kulima bustani, haya yote yanasababisha baadaye ashindwe kufanya kazi ya aina yoyote," alisema.

Tatizo lingine analitaja kuwa ni kwa watoto wanaosoma shule za mjini, kazi si sehemu ya malezi hivyo, na wenyewe wanafikiri kwamba atakuja na kukuta fedha na ndizo zitafanya kazi na si yeye.

Padre Kitima aliwakumbusha wazazi kuwa malezi ya mtoto ni lazima ajengewe hofu ya Mungu ili wajue neno Mungu si la kutamka tu bali linapaswa kuishi.

Pia alisema ni lazima wahakikishe wanafunda tabia za watoto wao ili wengine wamwone ana vigezo vya kijamii na kukubalika kila hatua ya maisha ya mtoto.

"Mtoto anapojitegemea wazazi huwatenga, mila na dini hutengwa ndiyo maana unakuta vijana wengi wanashindwa kuanzisha familia na wanaoanzisha wanakimbia," alisema.

**KUVUNJIKA NDOA**

Alisema kuvunjika kwa ndoa nyingi kunasababishwa na kutofuata taratibu za kimila za kuanzishwa familia na maandalizi ya malezi yanayoanza utotoni ikiwamo jando ambalo hutumika kuwaandaa kuwa wanaume thabiti wanaoweza kuwajibika kutunza ukoo na kabila.

Chifu Mkuu wa Wasafa kutoka Mbeya, Loketi Mwashinga, alisema kwa sasa limekuwa jambo la kawaida kumkuta kijana mwenye umri mdogo, akilelewa na mwanamke mtu mzima na akiwa hana wasiwasi wowote.

Alisema wanafanya hivyo kwa sababu hawataki kujishughulisha zaidi ya kutafuta urahisi wa maisha kwa wanawake waliowazidi umri au wenye umri wao ambao wana uwezo wa kipato.

Chifu Mwashinga alisema vijana wa sasa wamekuwa tofauti na mila zilizowalea wazazi wao na kilichowafikisha kuwa hivyo ni utandawazi.

"Ili kuwarudisha kwenye mstari ni lazima serikali ikubali kushirikiana na wazee wa mila kila mkoa ambao wao watasaidia kuelimisha na kukemea vitendo vinavyofanywa na vijana tofauti na mila na desturi, wakati mwingine unaweza kuogopa kukemea maana wana lugha chafu na wanaweza kukupiga.

"Maadili ya watoto yanaanzia kufundishwa nyumbani, walimu wanapokea pamoja na jamii. Kuna tukio hapa Mbeya lilitokea shule moja ya sekondari ilikuwa inaongoza kwa matukio ya mimba. Tuliposhirikishwa tulitoa kauli moja kwamba mtoto atakayempa mimba binti, tutamhamishia ailee wakati binti akiendelea na masomo, mpaka sasa hakuna mimba tena" alisema.

Mwenyekiti wa Kamati za Amani na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Shekhe Alhad Mussa Salim, aliwakumbusha wanaume kwamba jukumu walilobeba ni la kumsimamia mwanamke ikiwa ni pamoja na kutimiza wajibu wa kumlisha, kumvisha na kumpatia makazi.

"Mwanamke akifanya majukumu hayo huwa ni hisani si wajibu wake na anapofanya hivyo hupata dhawabu , kitendo cha mwanaume kuanza wajibu wake anapoteza heshima yake", alisema huku akitoa wito kwa vijana kwamba wasikwepe majukumu yao na kutafuta kulelewa.

Jumanne Hassan, mkazi wa Mwenge mkoani Dar es Salaam, alisema kitendo cha baadhi ya vijana wa kiume kutowajibika kwenye majukumu ya familia au kujishughulisha kinasababishwa na kupenda maisha rahisi.

"Siku hizi vijana hawataki kutumia akili nyingi, hawataki kutumia nguvu. Wanataka maisha rahisi, walelewe. Wakiwa na familia jukumu la malezi wanaliacha kwa mwanamke.

Unakuta mwanamke anaamka alfajiri anakwenda sokoni ananunua maembe anaweka kwenye beseni anatembeza barabarani anauza, mwanaume anaamka saa tano, anataka akute chai mezani akinywa anaishia kijiweni," alisema.

Fransisca Peter mkazi wa Tegeta, Dar es Salaam, ambaye ni mama mwenye watoto watatu wakiwamo wawili wa kiume, alikiri kwamba wazazi wengi wamesahau malezi na kufanya watoto wajilee kupitia mitandao ya kijamii matokeo yake yanaonekana hivi sasa.

# Othman ataka ufumbuzi kupanda kwa bei za bidhaa mwezi mtukufu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameziagiza Mamlaka na Taasisi zinazosimamia biashara na masoko kukaa pamoja ili kujadili matatizo yanayochangia baadhi ya bidhaa kupanda bei hasa katika kipindi cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Othman ameyasema hayo jana katika soko kuu la Darajani mjini Unguja, baada ya kukamilisha ziara yake ya kutembelea masoko ya bidhaa mbalimbali Zanzibar kuona mwenendo wa bei na upatikanaji bidhaa tofauti hasa kwa mahitaji ya futari ya mfungo wa Ramadhani.

Alisema katika ziara hiyo, amebaini kwamba kuna baadhi ya matatizo yaliyochangia kuwapo bei kubwa kwa baadhi ya bidhaa na pia mpangilio wa bei za bidhaa usiowiana kwa bidhaa mbalimbali hata zile zinazotoka Tanzania Bara. Alisema jambo hilo linaweza kupatiwa ufumbuzi na mamlaka na vyombo hivyo baada ya kukaa pamoja.

Kiongozi huyo alisema serikali katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu inataka kuwapo unafuu wa bei za bidhaa tofauti masokoni hasa zinazotumiwa zaidi na wananchi kwa futari ili wazimudu na kuendelea na ibada ya swaumu kwa wepesi zaidi kwa upatikanaji wa mahitaji yao ya futari.

Kwa mujibu wa Othman, kuna changamoto ya kupanda bei za baadhi ya bidhaa, hivyo kuwapa ugumu baadhi ya wananchi kutomudu upatikanaji wa mahitaji jambo ambalo watendaji kupitia mamlaka na taasisi husika wanapaswa kulijadili na kuona namna ya kuzitatua.

Pia alisema katika ziara hiyo amebaini kwamba kuna masuala ya kibiashara ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi na serikali jambo ambalo litawezesha kupatikana unafuu wa bei za bidhaa kwa wananchi.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, aliyembatana na Othman katika ziara hiyo, alisema serikali imekuwa ikijitahidi kuweka mazingira mazuri na rafiki ya kibiashara kama vile kupatikana kwa maeneo ya biashara ambayo yatasaidia kufanya biashara kwa wepesi.

Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban, alisema kwamba wizara hiyo imekuwa ikiwezesha kuzifanyia kazi changamoto mbalimbali za kibiashara ili kuweka uwiano wa bei kwa bidhaa mbalimbali na wananchi waweze kupata unafuu wa mahitaji yao. Baadhi ya wafanyabidhara wanaouza bidhaa zinazotoka Tanzania Bara, kikiwamo kitoweo cha nyama ya ng'ombe, wamesema kupanda kwa bei kunatokana na kuwapo tozo mbili za Tanzania Bara na Zanzibar, jambo ambalo walisema linawaongezea gharama watumiaji wa bidhaa hizo.

Kuhusu uhaba wa nazi, baadhi ya wafanyabishara walisema kupungua kwa kiasi kikubwa kwa bidhaa hiyo Zanzibar, tegemeo kubwa limekuwa Tanzania Bara hasa katika maeneo ya Lindi , Kilwa na Mafia lakini kumekuwa na tatizo la usafiri kufikisha bidhaa hiyo Zanzibar. Hali hiyo, walisema inaongeza bei na kuwafanya wananchi wenye kipato kidogo kushindwa kumudu.



Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Bakwata, Shekhe Hamisi Mataka (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya gazeti la Dar'sa la Kiislamu, Khalfan Mazrui, wakati wa uzinduzi wa gazeti hilo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wasota mwezi gesti kumsubiri Waziri Mkuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BAADHI ya wakazi wa kijiji cha Sale, Loliondo wilayani Ngorongoro mkoani Arusha, wamejikuta wakisota kwa takribani siku 30 katika nyumba ya kulala wageni jijini hapa, wakitaka kumwona Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Wakazi hao ambao waliwawakilisha wanakijiji wenzao, waliwasili jijini Dodoma tangu Februari 26, mwaka huu, kwa lengo la kumwona Waziri Mkuu ili kumfikishia malalamiko ya eneo la mashamba yao kumegwa na kijiji jirani.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, mmoja wa wanakijiji hao, Mary Sekeretu, ambaye aliwawakilisha kinamama, alisema lengo la kuja jijini Dodoma ni kuuona viongozi wa juu akiwamo Waziri Mkuu ili kufikisha malalamiko yao.

Sekeretu alisema kutokana na mgogoro huo wa mipaka baina ya kijiji chao na kijiji jirani cha Yasimdito kilimega eneo kubwa ambalo walikuwa wakilitumia kwa ajili ya kilimo kutokana na upimaji wa mipaka ya kiutawala uliofanywa na serikali.

"Mimi nimekuja Dodoma kutoka Loliondo kuwawakilisha kinamama wenzangu ambao wametutuma kuja kumwona Waziri Mkuu. Lengo letu ni kutoa malalamiko yetu kwa uongozi wa juu kutokana na wilaya kushindwa kutusaidia kupata haki. "Maeneo ambayo yamechukuliwa ni yale ambayo tulikuwa tukiyatumia kwa ajili ya kilimo lakini waliokuja kupima ardhi walipima bila kushirikisha pande zote mbili, hivyo kusababisha mashamba yetu kumegwa na kijiji jirani," alisema.

Sekeretu alisema kutokana na hali hiyo, hivi sasa wanashindwa kulima kutokana na upande wa pili kupiga marufuku ya wao kuingia kwa madai hilo si eneo lao tena hali ambayo inaweza kusababisha uvunjifu wa amani. "Sisi kama kinamama tumeona hakuna haja ya suala hili kuendelea kulifumbia macho kwani linaweza baadaye kuleta maafa kutokana na vijana kuanza kutaka kuvunja amani. Tunaiomba serikali ije ili kutupatia suluhu ya mgogoro huu," alisema.

Mwakilishi wa kundi la wazee, Steven Giranga, alisema toka wamefika Dodoma wamejaribu kufanya jitihada za kuonana na viongozi wa serikali lakini kila wanapofika wanagonga mwamba. "Baada ya kushindwa kumwona Waziri Mkuu, ikabidi tumtafute Waziri wa Ardhi, (Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula) lakini pia na yeye tumeshindwa. Tumekuja hapa kwa gharama za wananchi ambao wametuchangia kuja kuiona serikali ili kupata suluhu, hivyo tumeona ninyi waandishi wa habari mnaweza kutusaidia kufikisha kilio chetu hadi kwa Rais wetu Samia (Suluhu Hassan)," alisema. Mwenyekiti wa Kijiji cha Sale, Mussa Radia, alisema wanahofu kuwa mgogoro huo kama hautatatuliwa kwa wakati, kunaweza kuibuka mapigano baina ya pande hizo ndiyo maana waliona wafike Dodoma kuwaona viongozi wakuu wa nchi ili kupata suluhu.

"Cha ajabu tumefika Dodoma lakini hakuna tulichopata zaidi ya kutumia fedha kwa ajili ya malazi na usafiri kila siku kwenda mji wa kiserikali. Ndiyo maana tumeona leo (jana) kabla ya kuondoka tuzungumze na vyombo vya habari ili mtusaidie kufikisha kilio chetu," alisema Radia Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, hivi karibuni akifungua mafunzo ya uongozi kwa wakuu wa wilaya yaliyofanyika kwa siku tano jijini hapa, aliwataka kuhakikisha wanashughulikia malalamiko ya wananchi yanayohusu migogoro ya ardhi na mipaka ya vijiji.

## WB yataja mbinu kasi kukuza uchumi

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Dunia (WB) imesema serikali na sekta binafsi zinapaswa kushirikiana kwa ukaribu ili kukuza uchumi imara.

Mkurugenzi wa WB Tanzania, Nathan Belete, alitoa rai hiyo jana wakati wa mkutano ulioandaliwa na Jukwaa la Maofisa Watendaji Wakuu wa Kampuni Binafsi (CEOrt), ikiwa ni sehemu ya kikao cha kila mwezi.

Katika mkutano huo uliowashirikisha wakuu wa sekta binafsi uliolenga kujadili mtazamo wa Tanzania, Belete alisema ushirikiano wa pamoja kati ya serikali na sekta binafsi unahitajika ili kuongeza kazi ya ukuaji uchumi.

"Benki ya Dunia inatamani kuona hatua za kuwajibika kutoka kwa sekta binafsi katika kukuza biashara, kuzalisha ajira nyingi hususani kwa vijana pamoja na kuongeza thamani ya uzalishaji, lengo ni kufikisha uchumi wa Tanzania kwenye asilimia saba," alisema.

Alisema WB itaendelea kufanya kazi na mamlaka husika kwa mashauriano ya karibu na sekta binafsi, lengo kuu ni kuboresha mazingira ya biashara, akisema ni lazima kuwapo na mazingira wezeshi ya biashara ili sekta binafsi iweze kujiendeleza. Kadhalika Belete alisema WB inaamini katika sekta binafsi iliyoimarika, kwamba wanaipongeza serikali kwa kufanya mageuzi ambayo yanaunga mkono sekta binafsi.

"Hali ya uchumi wa Tanzania ni thabiti, kasi ya ukuaji wake kwa mwaka jana ilikuwa ni asilimia 4.6, ina tia matumaini na ni kielelezo cha uhusiano mzuri kati ya serikali na sekta binafsi," alisema Belete.

Naye Mwenyekiti wa CEOrt, David Tarimo, alisema sekta binafsi wanawajibu wa kujadiri kuhusu matatizo na kanuni za sera, masuala ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

"Sekta binafsi ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi. Tukiweka njia sahihi ya kuwezesha utendaji wa sekta hiyo kasi ya ukuaji uchumi kufikia asilimia saba inaweza kufikiwa," alisema.

Tarimo alisema idadi ya watu inaongezeka, hivyo nchi inatakiwa kuwa na ukuaji halisi wa matumaini wa kila mtu kwa kuwekeza katika elimu na afya.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za WB, uchumi wa Tanzania umeonyesha kuimarika baada ya mlipuko wa ugonjwa wa corona.

RIPOTI MAALUM

# Kasi watoto kuzaliwa na maradhi yaongezeka

**Na Waandishi Wetu**



Watoto wenye ulemavu wa akili na usonji katika kituo cha Udiakonia, kilichoko Mtoni, Dar es Salaam.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

MIAKA ya karibuni limekuwapo tatizo la kinamama kujifungua watoto wenye magonjwa yasiyoambukiza, hivyo kuiweka nchi kwenye hatari kubwa ya ongezeko la wagonjwa na ukosefu wa nguvu kazi.

Uchunguzi wa Nipashe umebaini kuwa tatizo hilo linazidi kushika kasi kulinganisha na miaka ya nyuma na kwamba baadhi ya magonjwa hayo yalikuwa yakiwapata watu wazima. Hali hiyo imeilazimu Nipashe kupiga hodi kwa madaktari bingwa ili kufahamu nini kisababishi kikuu.

Mtaalamu wa magonjwa ya watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Boniface Mariki, amesema ziko sababu mbalimbali zinazofanya watoto kuzaliwa wakiwa na magonjwa yasiyoambukiza.

Dk. Mariki alisema baadhi ya magonjwa ambayo watoto wanazaliwa nayo ni pamoja na kisukari, mgongo wazi pamoja moyo.

Alisema moja ya sababu ni pamoja na kinamama kutohudhuria kliniki wakati wa ujauzito, hivyo kukosa elimu pamoja na baadhi ya dawa muhimu ambazo wanatakiwa kuzitumia.

Baadhi ya watoto, alisema wanazaliwa na kisukari kutokana na kurithi ugonjwa huo kutoka kwa mama au kupata maambukizi ambayo yanashambulia kongosho, hivyo kushindwa kuchuja sukari.

"Watoto kuzaliwa na matatizo ya mgongo wazi na kichwa kikubwa husababishwa na kinamama kutofuata masharti wanayopewa na wataalamu hospitalini wakati wa ujauzito hasa kumeza vidonge vya kuongeza damu na madini ya folic acid," alisema Dk. Mariki.

**UVUTAJI SIGARA**

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake, Dk. Cosmas Kapinga, anabainisha kwamba sababu zinazosababisha mtoto kuzaliwa na magonjwa yasiyoambukiza ziko nyingi kama vile kurithi, ukosefu wa lishe kwa mama mjamzito au mtoto.

Alisema sababu nyingine ni jamzito kuvuta sigara wakati wa miezi mitatu ya ujauzito hali inayoweza kusababisha mtoto kuzaliwa na tatizo la moyo, presha au kisukari.

"Hata matumizi ya pombe kwa mama mjamzito, matumizi ya dawa za kulevya, matumizi ya dawa za malaria, minyoo kipindi cha miezi mitatu ya ujauzito yanaweza kusababisha mtoto kuzaliwa na magonjwa yasiyoambukiza," alisema Dk. Kapinga.

Dk. Kapinga alisema sababu nyingine ni majeraha kwa mjamzito wakati wa kujifungua, kwamba anaweza kumbana mtoto kichwa na kusababisha mtoto huyo kuzaliwa akiwa taahira.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake kutoka Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), Dk.Harry Mwambe, anaeleza kuwa kinamama kuwa na tatizo la sukari ni moja ya sababu ya kuzaa watoto wenye ugonjwa huo.

"Shida kubwa ni kinamama wengi hivi sasa kuwa na shida ya sukari nyingi, hivyo mtoto anapozaliwa ana 'adopt' hali ile ndiyo maana unakuta hivi sasa kumekuwa na tatizo la idadi kuwa ya watoto wadogo kuwa na shida ya ugonjwa wa sukari," alisema.

Alibainisha kuwa mtindo wa maisha nao umekuwa chanzo kikubwa cha kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

"Hivi sasa watu wanakula hovyo vyakula unakuta mtu ana uzito mkubwa kuliko urefu wake, hivyo inatakiwa watu kuanza kula vyakula salama lakini pia kufanya mazoezi ili kuondokana na tatizo hili la magonjwa yasiyo ya kuambukiza," alisema Dk. Mwambe.

Dk. Salha Nassoro Rashid kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara alisema miongoni mwa magonjwa ambayo watoto wanazaliwa nayo ni vichwa kujaa maji, utumbo kuwa nje na kuzaliwa bila kuwa na sehemu ya haja kubwa.

Alisema tatizo la watoto kuzaliwa na vichwa maji maarufu vichwa vikubwa lipo kwa wingi huku akibainisha kuwa idadi yao si kubwa sana kwa mwezi, kwamba wanapokea mtoto mmoja na wengi wao wanakuwa wamepewa rufani.

Pia alisema kuhusu utumbo kuzaliwa ukiwa nje ni tatizo ambalo lipo na kwa wiki wanapokea watoto wawili.

Daktari kutoka Idara ya Upasuaji wa Ubongo na Mfumo wa Fahamu Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, David Kambale, alisema uzembe, ulaji wa vyakula, mtindo wa maisha ni chanzo cha magonjwa hatari kwa watoto.

Alisema ongezeko la watoto wanaozaliwa na matatizo mbalimbali ikiwemo magonjwa ya saratani, vichwa vikubwa pamoja na mgongo wazi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa vimekuwa vikisababishwa na tatizo la kinamama kutokujali mienendo ya maisha kila siku.

Alisema zaidi ya watoto 1,000 kutoka mikoa mbalimbali ya ndani na nje ya Kanda ya Ziwa hupokelewa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando wakiwa na magonjwa ya saratani, vichwa vikubwa na mgongo wazi. Alisema hizo ni takwimu kuanzia Oktoba, 2021 hadi Oktoba, mwaka jana.

Alisema ugonjwa wa kichwa kikubwa kitaalamu hujulikana kwa jina la 'Hydrocephalus' ikiwa jina hilo linatokana na neno la Kigiriki lenye maana ya maji ndani ya kichwa, alieleza kuwa si kila mwenye kichwa kikubwa ana 'hydrocephalus'.

Dk. Kambale alieleza watoto 700 hupokewa kwa mwaka katika hospitali hiyo ili kufanyiwa upasuaji, akisema tatizo hilo linatokana na ubongo kuwa na kiasi fulani cha majimaji.

Kuhusu tatizo la mgongo wazi, Dk. Kambale alisema ugonjwa huo kwa jina la kitaalam huitwa 'spina bifida', ambapo ni ugonjwa au hali ambayo mtoto anazaliwa nayo huku uti wa mgongo ukiwa wazi, kutokana na mifupa kutokufunga vizuri.

Alisema kwa kawaida baada ya mimba kutunga uti wa mgongo hutengewa nusu upande mwingine na nusu upande mwingine na baadae kuungana, kwamba wakati wa muunganiko huo ndiyo kasoro inaweza kutokea na hivyo sehumu fulani ikawa haijaziba vizuri na kuacha tundu.

Alisema tatizo hilo linaweza kusababishwa na mjamzito kufanyiwa kipimo cha mionzi (X-ray), matumizi ya dawa za kifafa, upungufu wa 'folic acid' yaani dawa za vitamin B9 zitolewazo katika zahanati wakati wa kliniki.

Pia alisema ugonjwa huo unaweza kumpata mtoto yeyote ambaye mama yake hakupata virutubisho kabla ya kushika mimba ikiwa kwa kawaida virutubisho hivyo hupatikana katika vyakula vyenye protini na vina uwezo wa kumzuia mama kwa asilimia kubwa asipate changamoto ya kuzaa mtoto mwenye ulemavu huo.

Daktari wa magonjwa ya saratani kwa watoto kutoka hospitalini hiyo, Dk. Heronima Joas, alisema ugonjwa wa saratani kwa watoto nao ni tishio nyakati hizi, huku sababu kubwa zikidaiwa kuwa pamoja na wajawazito kutumia samaki wanaovuliwa kwa kutumia kemikali aina ya zebaki zinazohusishwa na maambukizi ya saratani kwa mtoto kipindi akiwa tumboni.

Alisema mpaka sasa wataalamu bado hawajabaini sababu hali za magonjwa ya saratani kwa watoto, lakini kunavitu baadhi ambavyo vinahusishwa na ugonjwa huo ikiwa ni pamoja na uvuvi wa kemikali.

**Imeandaliwa na Jaliwason Jasson (BABATI), Paul Mabeja, (DODOMA), Vitusi Audax (MWANZA) na Nebart Msokwa (MBEYA)**

## HABARI KITAIFA

# Mchimba madini amwangukia Rais leseni

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MCHIMBAJI mdogo wa madini, Richard Lyamuya, mkazi wa Manispaa ya Singida , amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati apate haki yake baada ya Ofisi ya Madini Mkoa wa Singida kukataa kumpatia leseni wakati amefuata taratibu zote kwa kulipia ada za zaidi ya Sh. milioni moja zilizoainishwa kisheria.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Lyamuya alisema alipeleka maombi ya kupatiwa leseni ya uchimbaji dhahabu katika kijiji cha Matongo wilayani Ikungi na ofisi ya Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Singida ilimwelekeza alipie ada ya maombi, ada ya maandalizi na ada ya pango na vyote alilipia kama kawaida na kupewa stakabadhi.

Lyamuya alisema katika hali ya kushangaza, baada ya leseni kutoka ili akabidhiwe, Ofisa Madini Mkazi Mkoa, Chone Malembo, amekataa kutoa saini leseni ili itoke kwa madai kwamba eneo aliloomba lina mgogoro.

Kutokana na hatua hiyo, alisema kumekuwa na maswali yasiyo na majibu kwa sababu kama ofisi hiyo ilijua eneo hilo lina mgogoro, kwa nini ilimruhusu kulipia ada hizo.

Alisema amefuatilia suala hilo kwa kuandika barua katika ofisi ya madini mkoa wa Singida, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi na kwa Mkuu wa Mkoa lakini hajapata msaada wowote.

"Katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi nimefika zaidi ya mara saba bahati mbaya sikufanikiwa kuonana na mkuu wa wilaya badala yake nilionana na Katibu Tawala ambaye alinisikiliza na akanipa majibu kuwa amezungumza na Ofisa Madini wa Mkoa akasema leseni ninayoilalamikia hataweza kunipa bali niendelee na leseni zingine nilizo nazo," alisema.

Aliongeza kuwa jambo la kushangaza wakati tayari ameshafanyiwa mchakato na kusubiri kupata leseni, baadhi ya maofisa katika ofisi ya madini mkoa wa Singida waliweka ombi namba PML145961/CZ Septemba 3, mwaka jana, kwenye mtandao katika eneo hilo hilo ambalo yeye ameomba leseni lakini baadaye ombi hilo liliondolewa.

Lyamuya alisema baada ya kufika katika ofisi zote za serikali bila mafanikio, Machi 13, mwaka huu, mwanasheria wake wa kampuni ya Kim & Co. Advocates, aliiandikia barua ofisi ya madini mkoa kutaka mteja wake apewe leseni yake kwa kuwa amefuata taratibu zote.

"Unachokifanya si matakwa ya sheria bali ni utashi wako kama mtu binafsi. Hakuna mgogoro wa kiuchimbaji katika leseni hii na hata mgogoro ungekuwapo basi kifungu cha 102 cha Sheria ya Madini namba 14 ya 2010 kingetumika na kwa niaba ya Kamishina wa Madini ungeendesha nafasi hii ya kimahakama na kutoa uamuzi wa mgogoro. Lakini tunachokiona unashughulika na upande mmoja wa mteja wetu," imeeleza sehemu ya barua hiyo ya mwanasheria ambayo ameandikiwa ofisa madini mkazi.

Mwanasheria wa mchimbaji huyo, Raymond Kim, ameendelea kueleza katika barua yake hiyo kwa kutoa angalizo kwamba mteja wao atawajibika kuchukua hatua za kisheria kama ofisi ya madini mkoa itaendelea kukataa kutoa leseni namba PML 0734SGD ambayo leseni hiyo ilitokana na ombi namba PML 133372/CZ.

Pamoja na kuliweka katika mizania ya kisheria, mchimbaji huyo amemwomba Rais Samia aingilie kati suala hilo kwa kuwa amefuatilia katika ofisi nyingi za serikali na hajapata msaada.

Kaimu Ofisa Madini Malembo alipoulizwa alikiri kuufahamu mgogoro huo na kuwa ulianza baada ya watu wawili kujitokeza kwamba eneo hilo aliloomba leseni Lyamuya (mchimbaji) ni shamba lao.

Alisema walibaini eneo hilo lina mgogoro wakati tayari ameshafanya mchakato wa malipo. Alipoulizwa na waandishi kama je, fedha hizo atarudishiwa mchimbaji huyo, alijibu kuwa hilo ni suala lingine bila ya kufafanua zaidi.

Malembo alisema ofisi yake itaendelea kufanya mchakato wa kusuluhisha kati ya wenye shamba ambao nao wanataka wafanye uchimbaji kwenye eneo hilo kama wataona inafaa wafanye ubia wa uchimbaji.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, akiagana na Kamishna wa Maadili, Jaji Mstaafu, Sivangilwa Mwangesi, mara baada ya kufungwa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma jijini Dodoma jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi maadili ya umma wasisitiza weledi

**Na James Mwanamyoto,**
DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama awewataka watumishi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuyafanyia kazi kwa uadilifu, weledi na busara malalamiko yanayowasilishwa na wananchi dhidi ya viongozi wa umma.

Mhagama alitoa maelekezo hayo juzi wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, mjini hapa.

Waziri Mhagama aliwasisitiza watumishi hao kutenda haki katika kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa na wananchi dhidi ya viongozi wa umma.

"Tendeni haki kwani kutenda haki ni pamoja na kumwadhibu aliyebainika kufanya kosa na kutokumwadhibu ambaye hajafanya kosa. Hizo zote ni haki kwa muktadha wa maadili na utawala bora," alisema.

Mhagama alisema ili taifa lisonge mbele, linahitaji mchango wa kiutendaji wa watumishi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambao wana jukumu kubwa la kuwaongoza Watanzania kuliletea taifa maendeleo kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Pia alizitaka taasisi zote za umma kufanya mikutano ya mabaraza ya wafanyakazi kwa mujibu wa Waraka Na. 1 wa Rais wa Mwaka 1970 unaoendelea kutumika mpaka sasa.

"Taasisi zingine zimekuwa zikipanga bajeti bila kufanya mikutano ya mabaraza ya wafanyakazi. Hiyo ni kuwanyima haki watumishi kutoa maoni na michango yao itakayowezesha utekelezaji mzuri wa bajeti.

"Hatua ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kufanya mkutano wa baraza la wafanyakazi ili kutathmini utekelezaji wa bajeti, kinaashiria kuwa taasisi inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya maadili.

Kamishna wa Maadili, Jaji Mstaafu Sivangilwa Mwangesi, alisema mkutano huo wa baraza la wafanyakazi ni wa pili kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2022/23. Kwa mujibu wa utaratibu wa taasisi yake, ni mkutano maalum kwa ajili ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 utakaofikia tamati Juni 31, mwaka huu, pamoja na kujadili mpango mkakati wa kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2023/24.

## Chuo kufumua mitaala kuendana na hali halisi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

CHUO Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), kimeanza rasmi mchakato wa kukusanya maoni ya waajiri katika bodi zinazosimamia taaluma na utaalam, sekta ya umma na binafsi, wahitimu na wanafunzi, kabla ya kuifumua mitaala 15 na kuandaa programu mpya 11 zitakazoamua hatima ya wanaohitimu elimu ya juu kukabiliana na soko la ajira. Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Alfred Sife, wakati anazindua mpango huo juzi, alisema hatua hiyo ni muhimu katika kipindi ambacho soko la ajira limebadilika, kwa maana ya kuwa na mahitaji mapya ya ujuzi na maarifa.

Prof. Sife alisisitiza kuwa hatua hiyo inachagizwa pia na mwingiliano wa ajira kwa mataifa mbalimbali kutokana na utandawazi, idadi ya wahitimu kuongezeka kupita uwezo wa nafasi za ajira zinazozalishwa na sekta mbalimbali.

"Tuko katika kipindi kijulikanacho kama mapinduzi ya viwanda yanayoongozwa na matumizi makubwa ya TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), hivyo kuhitaji uzalishaji wa wahitimu wenye ujuzi na mapinduzi haya,"alisema.

Kabla ya uzinduzi huo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Utawala na Fedha wa MoCU, Prof. Fredy Kilima, alisema maboresho hayo ni utekelezaji wa mradi wa kitaifa wa elimu ya juu wa mageuzi ya kiuchumi.

Mradi huo unaotekelezwa katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, ni sehemu ya vyuo vingine 14 vilivyoko hapa nchini.

"Mradi unafadhiliwa na serikali ya Tanzania chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB). Dhima kuu ya mradi huu ni kuwa na elimu inayoendana na soko la ajira.

"Kimkakati kuna namna nyingi za kufikia lengo hili ili kutimiza dhima ya mradi mojawapo ya mikakati iliyopendekezwa na mradi, ni kufanya marejeo ya mitaala iliyoko na kuandaa mitaala itakayowawezesha wahitimu kuwa na ufahamu na maarifa yatakayoleta tija kwenye soko la ajira," alisema.

Aidha, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, anayeshughulikia taaluma, utafiti na ushauri elekezi, Prof. John Safari, akizungumzia maboresho hayo, alisema: "Umuhimu wake unaonekana katika elimu tunayoitoa inaakisi mahitaji ya wakati ya kijamii na kiuchumi.

"Tunafanya hivyo ili kuhakikisha kwamba tunajibu hoja ya changamoto mbalimbali za kijamii na kwa hiyo maoni yanapaswa kutoka kwa jamii yenyewe ambayo ni Watanzania wenzetu."

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jitihada za pamoja kichocheo katika kutokomeza kifua kikuu

**MACHI** 24 kila mwaka, huwa ni maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu na kwa mwaka huu, kitaifa yalifanyika Bariadi mkoani Simiyu na mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Katika hotuba yake, Waziri Mkuu alisema ugonjwa huo umeendelea kuwa tishio duniani hususani kwa nchi zinazoendelea, Tanzania ikiwamo. Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Majaliwa, wastani wa watu 28,000 hufariki dunia kila mwaka kutokana na ugonjwa huo. Pamoja na hali kuwa hivyo mpaka sasa, vifo hivyo kwa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), kwa mwaka 2022 vilipungua kutoka 55,000 hadi 25,800 sawa na asilimia 55.

Pamoja na kubainisha hayo, ziko habari njema kwamba maambukizi mapya ya ugonjwa huo hapa nchini yamepungua kutoka wagonjwa 306 katika kila watu 100,000 hadi wagonjwa 208 katika idadi hiyo ya watu. Kupungua kwa maambukizi hayo kunatokana na jitihada za makusudi zilizofanywa na serikali pamoja na wadau wengine katika kuhakikisha ugonjwa huo unakuwa si tishio tena.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na serikali na wadau hao ni pamoja na kuongeza wigo wa huduma ili kuwafikia wananchi hususani maeneo yenye maambukizi makubwa ya kifua kikuu.

Sambamba na jitihada za kuwafikia wananchi na kutoa elimu, kupungua kwa maambukizi na vifo kunatokana na dhamira ya serikali ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya ili kumwezesha kushiriki ipasavyo kwenye shughuli za uzalishaji mali na kujikwamua na umaskini kupitia mkakati wa dunia wenye lengo la kuhakikisha kifua kikuu kinatokomezwa ifikapo 2030.

Jitihada zinazofanywa katika kuhakikisha azma ya kutokomeza kifua kikuu mwaka 2030 hazitakuwa na maana kama kila Mtanzania hatashiriki kwa nafasi yake na eneo lake katika kampeni hiyo. Jambo la kwanza, inapaswa kutolewa elimu kuhusu ugonjwa huo kwa kuelezea dalili zake pamoja na kuhamasisha iwapo kampeni kwa ajili ya upimaji wa hiari wa kifua kikuu.

Jambo lingine linalopaswa kuzingatiwa ni kuelimisha jamii kuondokana na mila potofu zilizotamalaki katika jamii kuwa mtu akipata kifua kikuu anakuwa amelogwa hatua hiyo husababisha baadhi ya watu kwenda kwa waganga wa jadi kupiga ramli kumtafuta mchawi na matokeo yake kunakuwapo na uhasama, chuki na mauaji kwa wanaodaiwa kutenda vitendo hivyo. Watu ni lazima waelimishwe kwamba ugonjwa huo unatibika pindi mtu anapoupata.

Inafurahisha kuona kwamba katika maadhimisho ya mwaka huu, umezinduliwa mkakati wa uwajibikaji wa pamoja wa kisekta katika kupambana na kifua kikuu. Mkakati huo uwe dira katika kushirikisha wadau wote wa kisekta kuhakikisha azma iliyokusudiwa inatimizwa.


Katika moja ya mikakati hiyo, kila Mtanzania ana wajibu wa kuhakikisha anachukua hatua zote za tahadhari kwa kuwa mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ambaye hajagunduliwa na kuwekwa katika utaratibu wa matibabu, ana uwezo wa kuambukiza watu kati ya 10 mpaka 20 kwa mwaka. Kwa hiyo elimu kuhusu kifua kikuu inapaswa kuwa shirikishi kwa maana ya wizara, idara na taasisi za serikali. Wadau wakuu wanaopaswa kuongoza kampeni hiyo ni Wizara ya Afya na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Msisitizo mkubwa unapaswa kuwa katika maeneo ya shughuli za kiuchumi kama vile madini, viwanda na uchorongaji na upasuaji wa udongo. Katika maeneo hayo, kuna vumbi jingi ambalo huathiri watu na kusababisha kuugua kifua kikuu. Pia suala la ujenzi wa makazi bora linahitaji kupewa msukumo mkubwa zaidi kwa sababu kukosekana kwa hewa ya kutosha ni chanzo pia cha ugonjwa huo.

Ni dhahiri kwamba kama kila mmoja atachukua hatua ya kuhakikisha anashiriki kwa nafasi yake, kuna uwezekano mkubwa mwaka 2030 usifike kwa Tanzania kutimiza malengo ya kutokomeza ugonjwa huo. Tanzania bila kifua kikuu inawezekana, iwe ndiyo kauli mbiu na dira katika kuelekea kwenye malengo hayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Miaka mwili bila JPM, miradi aliyoacha inaendelezwa

**LEO** ni siku ya tisa ya mwaka wa tatu bila kuwa na Rais John Magufuli, aliyefariki dunia Machi 17, 2021 akiwa mwenye ndoto ya kuhakikisha Tanzania inajitegemea kiuchumi.

Rais Magufuli aliondoka akiwa ameacha alama kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo aliyokuwa ameianzisha ikiwamo bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, reli ya kisasa, kuimariaha miundombinu ya barabara, ujenzi wa barabara za juu Dar es Salaam na mingine mingi.

Juhudi za kuboresha miundombinu ya barabara, zilisaidia kupunguza foleni jijini, ambazo kwa namna moja au nyingine zilichangia kukwamisha shughuli za kiuchumi.

Lakini pia aliamini kuwa kufanya kazi kwa nguvu, juhudi na maarifa, inawezekana watu kujiletea maendeleo, huku akizuia vijana kushinda vijiweni badala yake wafanye kazi, ili kujiletea maendeleo.

Ikiwa ni siku ya tisa tangu kumalizika kwa miaka miwili ya kifo chake na pia siku ya saba tangu kuanza mwaka wa tatu wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, ni vyema kutambua juhudi za viongozi hao katika kuleta maendeleo ya nchi.

Rais Magufuli hayupo tena, lakini bahati nzuri ni kwamba, mrithi wake naye anapita katika nyayo zile zile, kwa kuendelea kusimamia miradi aliyoanzisha mtangulizi wake, ili kuhakikisha inakamilika.

Miongoni mwa miradi hiyo nimeitaja awali kuwa ni bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa reli ya kisasa, ujenzi wa miundombinu ya barabara zikiwamo za juu, za mabasi ya mwendokasi na mingine katika maeneo mbalimbali nchini.

Rais Samia amekuwa akisisitiza kuwa serikali ya awamu ya sita inaendelea kukamilisha miradi yote ya maendeleo iliyoanza wakati wa serikali ya awamu ya tano na kwamba miradi mingi imeanza kukamilika.

Mkazo wa Rais kwa wananchi ni kuwataka wananchi kuhakikisha wanatunza miundombinu inayojengwa na serikali, ikiwamo barabara na madaraja ili iweze kudumu na kuchangia katika maendeleo ya taifa.

Anaweka wazi kuwa serikali haitawafumbia macho watendaji 'wanaopiga dili' katika miradi ya maendeleo na kusababisha wakandarasi wasiokuwa na sifa kupata kazi au kupitisha miradi iliyo chini ya viwango vinavyotakiwa.

Ninadhani kwamba kila mmoja wetu anahusika katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inaimarika kwa watendaji kuisimamia vizuri na pia wananchi kuwa tayari kutoa kwa vyombo vya dola wanapoona miradi inahujumiwa.

Pamoja na hayo, wakaguzi wa miradi hawana budi kujiweka mbali na rushwa kutoka kwa makandarasi ili wasipitishe miradi mibovu ambayo inaweza kuliingiza taifa kwenye hasara zisizotarajiwa.

Kimsingi ni kwamba, iwapo kila mmoja wetu atafanya sehemu yake kwa uaminifu, itakuwa ni rahisi kwa serikali kufikia malengo ambayo imejiwekea kwa ajili ya maendeleo ya taifa na watu wake.

Maana yake ni kwamba hakutakuwa na wachakachuaji wa miradi hiyo, wala watu wanaoiba miundombinu ya miradi yenyewe, kwani kwa hatua hiyo, itakuwa ni rahisi taifa kusonga mbele kimaendeleo na kiuchumi.

Kile ambacho Rais amekuwa akitamani, ni kuona utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaofanywa katika maeneo mbalimbali nchini, unakwenda sambamba na ukusanyaji wa mapato ili kukuza uchumi wa nchi.

Ukweli ni kwamba Rais anachukizwa na rushwa, ubadhirifu wa fedha, katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwani vitendo hivyo vinaweza vikavuruga jitihada za serikali za kuinua uchumi wa nchi.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Tumuunge mkono Samia kutafuta suluhu ya migogoro



Pascal Mayalla

KATIKA safu hii, leo naendelea na sehemu nyingine ya makala ya umuhimu wa usuluhishi kunapotokea mgogoro wowote badala ya kukimbilia mahakamani kufungua shauri la kesi za madai ambazo huchukua muda mrefu kusikilizwa na kutumia gharama kubwa.

Baada ya Rais wetu, Samia Suluhu Hassan, kuliishi jina lake la Suluhu kwa kuleta suluhu ya mtanziko wa kisiasa nchini, ni wakati mwafaka sasa kwa Watanzania kuanza kutumia njia ya usuluhishi kutatua migogoro yoyote, iwe ya kisiasa, kiuchumi au kijamii. Tunapokuja kwenye jambo lenye maslahi kwa taifa, upinzani si uadui. Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wapinzani ni kitu kimoja, hivyo katika kuzienzi nguzo zetu za umoja, amani na mshikamano, wanapaswa kukaa chini na kulitatua kwa njia ya maridhiano. Jambo hilo kwa kukaa pamoja, linaweza kuchukua muda usiozidi siku 30 tu wakati kesi zinakwenda miaka kwa miaka.

Usuluhishi ni mfumo wa utatuzi wa migogoro hususan ya kibiashara kati ya pande zilizo na mkataba kwa kusimamiwa na mtu au taasisi ambazo si mahakama lakini kwa kuzingatia taratibu zilizorahisishwa za kimahakama. Uamuzi unaotolewa katika usuluhishi unaitwa tuzo za usuluhishi (arbitral award). Usuluhishi ndio njia bora zaidi katika utatuzi wa migogoro kuliko mfumo wa kimahakama kwa kuwa mfumo wa usuluhishi unafanya yafuatayo;-

Kwanza, usuluhishi unawezesha utatuzi wa migogoro kwa njia ambayo ni ya haraka, kirafiki na yenye ufanisi zaidi, hivyo kuchukuliwa kuwa unaboresha mazingira ya ufanyaji biashara au jambo lolote linaloleta mvutano baina ya pande husika. Pili, usuluhishi unawezesha usiri (confidentiality) wa taarifa za wahusika kwa kuwa mfumo huu haufanyiki kwa uwazi.

Tatu, katika usuluhishi kuna uwezekano wa kupata watatuzi ambao wana utaalamu mahususi katika eneo lenye mgogoro unaotatuliwa, kuliko hata mahakama ambayo inazingatia tu sheria inasemaje. Nne na mwisho, lakini si kwa umuhimu, taratibu za uendeshaji wa mashauri ya usuluhishi zinaweza kubadilishwa, hivyo ziko 'flexible' na kunakuwa na 'flexibility' kuliko taratibu za mahakama.

Umuhimu huu wa kutatua migogoro kwa usuluhishi, umesisitizwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, mbele ya Rais Samia aliyekuwa mgeni rasmi, wakati wa Siku ya Sheria kwa mwaka huu, iliyoadhimishwa katika viwanja vya Chinangali, Dodoma.

Katika maadhimisho hayo, Jaji Mkuu Prof. Juma, alizungumzia umuhimu wa utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi unaofanana kabisa na falsafa ya maridhiano, ustahimilivu na mabadiliko ya kujenga upya nchi inayofanywa na Rais Samia.

Akisisitiza hilo, Jaji Mkuu alisema: "Sina budi kutambua na kuupongeza uongozi wako katika kukuza majadiliano na maridhiano katika siasa za Tanzania. Wewe, Mheshimiwa Rais, mapema mara baada ya kuingia madarakani Machi 18, 2021 ulianza kuhimiza mazungumzo, majadiliano na usuluhishi kwenye migogoro ya kisiasa. Ulionyesha dhamira ya dhati ya kuleta maridhiano kwa kuunda kikosi kazi cha kukusanya maoni. Ulisema kwamba, busara zilikutuma, baada ya kuona haja ya kufanya taifa liwe kitu kimoja, wote tuzungumze lugha moja; na ili taifa liwe moja, uliendelea kusema, ni lazima kuwapo mazungumzo na maridhiano kwenye vyama vya siasa."

Jaji Mkuu aliendelea: "Mheshimiwa Rais, uliita juhudi zako kuwa falsafa ya kusimamia maridhiano, ustahimilivu na mabadiliko ya kujenga upya nchi katika nyanja za siasa. Hapana shaka yoyote falsafa hiyo ndiyo iliyojengewa misingi elekezi kwa Mahakama chini ya Ibara ya 107A (2)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inayoagiza Mahakama za Tanzania kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa kuzingatia sheria; na katika kuzingatia sheria za nchi, Mahakama zinatakiwa kufuata kanuni elekezi ya kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro."

Hapa Jaji Mkuu amemwonyeshea Rais Samia kuwa mtu wa suluhu na si mtu wa kuendekeza migogoro ndiyo maana ameamua kutumia njia ya maridhiano ya kisiasa ili kupata suluhu ya jambo lolote lenye ukakasi. Katika kutafuta suluhu huko, anajikuta analiponya taifa dhidi ya baadhi ya majeraha yaliyosababishwa na utekelezaji sheria.

Kama Jaji Mkuu alivyompongeza Rais Samia kutafuta suluhu ya mtanziko wa kisiasa nchini kwa njia ya maridhiano, ikiwemo kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa, iliyozuiwa kinyume cha katiba na sheria. Katika kutafuta maridhiano, ukiishalitatua tatizo la mikutano ya hadhara sasa rukhsa, hakuna budi kwa wanasiasa na vyama vya siasa kuangalia mbele kwa moyo huo huo kama wa Rais Samia kwa kuruhusu mikutano ya siasa iendelee kwa kuangalia mbele na si kupoteza muda kuangalia nyuma nani alisababisha. Ari iwe daima mbele nyuma mwiko.

Hata kama kuna watu waliosababisha matatizo hayo, mafanikio ya usuluhishi na maridhiano ni kuwa na moyo wa kusamehe. Maadam sasa tumekubali kufungua ukurasa mpya wa maelewano na maridhiano, tuwasamehe wale wote waliosababisha, wawe wapo au hawapo. Kama wapo tuwasamehe kwa kuwa yaliyopita si ndwele tugange yaliyopo na yajayo na kama hawapo, wametangulia mbele ya haki, waachwe wapumzike kwa Amani. Si busara, si Uafrika, si Utanzania kutwa kucha kuwasema vibaya au kwa ubaya watu waliotangulia mbele za haki.

Moyo huu wa suluhu alio nao Rais Samia, kama lilivyo jina lake la Suluhu, haukuishia kwenye suluhu za kisiasa pekee, bali suluhu kiuchumi na kijamii, hivyo sasa tunajenga Tanzania njema, yenye amani, upendo, maelewano na ushirikiano, vitu vitakavyoharakisha sana maendeleo.

**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Paskali 0754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Ajira zisipopatikana figo zitanadiwa tu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

LENGO na madhumuni ya mzazi kusomesha mwanawe ni kumwondolea ujinga, kubwa likiwa kumwezesha kujikomboa kimaisha lakini pia kumsaidia mzazi kimaisha baadaye.

Hayo ndiyo yamekuwa maisha ya binadamu hususan sisi Waafrika kwamba unazaa mtoto, unamlea kwa chakula, malazi, mavazi na elimu na kumfanya akiba kwa ajili ya maisha ya siku zijazo.

Zamani watoto walizaliwa si kwa ajili ya kusoma bali kusaidia kazi za nyumbani na kuandaliwa kuwa warithi katika familia husika. Elimu ya darasani ilikuja baadaye.

Elimu hiyoililetwa na Wazungu ambao nao waliitumia kutawala akili zetu na hatimaye kutawala kimwili na kutunyonya walivyotaka. Ndiyo sababu elimu zamani ililenga zaidi Ulaya na si nyumbani.

Hata hivyo, baada ya sisi kupata wasomi kadhaa, tukaona umuhimu wa elimu kutokana na ukweli kwamba iliwawezesha wasomi kurithi kazi za wakoloni tuliowaondoa baada ya kujitawala.

Ndiyo sababu baada ya uhuru, elimu iliyotolewa ililenga kutukuza uzungu na wazungu, huku tukijifunza Historia na Jiografia ya Ulaya zaidi kuliko ile ya nyumbani.

Wanafunzi wa awali walimudu Kiingereza kwa kukisoma na kukiandika, hivyo kuwa sifa muhimu kwa msomi, lakini pia mfanyakazi. Bila kujua Kiingereza usingeajiriwa kokote.

Kwa kuwa wazazi walishaliona hilo kwamba bila elimu hususan ya Kiingereza mtoto asingeajiriwa, wakatilia mkazo mafunzo hayo ya kigeni zaidi kwa ajili ya ajira. Kwa mantiki hiyo, zamani mtoto alisoma si kwa lingine, bali kupata ajira katika ofisi za wazungu na hata baada ya Wazungu ilikuwa kwa ajili ya kupata ajira kwenye ofisi za watawala.

Wazazi walifurahi, kwamba watoto wao walipohitimu madarasa ya elimu ya msingi na sekondari, walikuwa na uhakika wa ajira ofisini na kuachana na uchungaji, kilimo, uvuvi na uganga wa jadi.

Kwa hiyo mtu alisoma akitarajia kumaliza na kuwa askari polisi, askari jeshi, mwalimu au karani ofisini. Yote hiyo, sifa ilikuwa kujua Kiingereza pamoja na ukakamavu.

Enzi hizo mtu asingeajiriwa mwalimu au karani kama hakujua kusoma au kuandika Kiingereza. Kasumba hiyo inaendelea katika baadhi ya ajira nchini.

Wakati huo ajira zilikuwa nyingi kutokana na idadi ndogo ya wanafunzi waliohitimu. Hivyo, hata mazungumzo yalikuwa kusoma na kuajiriwa, tofauti na sasa msisitizo mkubwa ni kusoma na kujiajiri.

Tunaambiwa hivi sasa elimu inayotolewa haiandai wahitimu kujiajiri ingawa mitaala ni ile ile iliyotumika zamani kuajiri. Pengine dhana ya uhakika ni kwamba nafasi za kazi si nyingi kulinganisha na wanaohitimu.

Na hiyo inatokana na kushindwa kubuni nafasi za ajira kwa kuanzisha miradi au kujenga viwanda ambavyo vingechukua wahitimu wengi wanaomaliza elimu za shule na vyuo.

Matokeo yake, vijana wanazurura mitaani na elimu zao vichwani na kujikuta wakijiingiza kwenye kamari, kujiuza na mbaya zaidi kuamua kuuza viungo vyao, ili kujipatia kipato cha kujikimu.

Wazazi kwa upande wao wanalalamika kugharimia watoto kwa hili na lile na baada ya kuhitimu wanarudishwa nyumbani kuanza upya wakiwa hawajui wanafanya nini kutokana na ukata unaozikabili familia zao.

Baadhi ya vijana, hivi sasa wamediriki kutangaza kuuza figo zao ili kuwezesha mikono kwenda vinywani na kugharimia mahitaji mengine. Wanapofanya hivyo hunyooshewa vidole kwamba ni kinyume cha sheria.

Wengine hususan wa kike, wanajiuza miili kwa lengo hilo hilo la kumudu maisha. Nao hali kadhalika wakifanya hivyo wanakodolewa macho na kuzomewa kwa kuwa wanapotoka.

Wako wanaojiingiza kwenye ushoga pia kwa malengo hayohayo ya kumudu maisha, huku baadhi ya mataifa yakishinikiza tabia hiyo chafu, lakini kwa mwenye njaa hilo hawezi kukiona bali maisha yake.

Viongozi kuendelea kushinikiza watu kujiajiri huku wakiwa hawana elimu ya kujiajiri, achilia mbali nyenzo za kutumia kwenye ajira hizo, ni kuwaonea vijana wao ambao wanajua kabisa wanaohubiri kujiajiri wameajiriwa.

Tunaona sasa angalau kwa mbali serikali inaanzisha mpango wa kilimo biashara kwa kuchukua vijana mitaani na kuwagawia mashamba kwa ajili ya ujasiriamali na kupunguza tatizo la ajira.

Ingawa kuna malalamiko kuwa vijana wanaochukuliwa si hasa walengwa, angalau jambo limefanyika ambalo baadaye litahitaji marekebisho ili vijana walengwa ndio wapewe fursa hiyo.

Lakini bado tunatakiwa kudhibiti chanzo cha matatizo ya vijana hususan ya ukosefu wa ajira badala ya kutibu matokeo yake ambayo ni matatizo endelevu kwao. **Alamsiki!**

# Siri iliyojifisha kuhusu uhaba wa chakula

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU za karibuni, wadau na wataalamu wa chakula barani Afrika, wamekuwa wakizungumzia uhaba wa chakula huku lawama nyingi zikielekezwa kwa Russia kuwa ndiyo chanzo.

Hata bila kuchambua sababu ya tatizo hilo, wataalamu hao wanarudia lawama hizo zinazoelekezwa kwa nchi za magharibi ilhali ziko sababu nyingi ambazo zimefanya hali kufikia ilipo sasa.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, Russia ni chanzo cha ukosefu au uhaba wa chakula kwa sababu tu imevamia Ukraine, bila kutafakari kwa kina kuwa kuna majanga mbalimbali kama ukame uliosababishwa na ukosefu wa mvua pamoja na mabadiliko ya tabianchi kuwa ni sababu pia.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Uhisiano kati ya Russia na Africa (Russia -Africa Relations), Vladimir Krasov, anasema Russia inalaumiwa kwa njaa itakayoenea duniani kote.

"Wakati huo huo wataalamu maarufu wa kimataifa wameshakiri hadharani kwamba sababu kuu ya mfumuko wa bei ya vyakula ni mabadiliko ya kiuchumi ya kiulimwengu, makosa ya kimfumo na kasoro za nchi za Magharibi za kutekeleza sera ya kiuchumi na ya kuhakikisha upatikanaji wa nishati na chakula. Majanga ya asili, mlipuko wa ugonjwa wa kuambukizwa na vikwazo vingi vya upande mmoja dhidi ya Russia vimezidisha mwelekeo huu mbaya vikitatanisha hali ya masoko ya kimataifa,, kwanza kabisa soko la bidhaa za kilimo.

Bei kubwa za nishati zilizosababishwa na nia ya nchi za Magharibi ya kuanza kutumia vyanzo vya nishati mbadala, ziliongeza gharama za usafirishaji," anasema Krasov.

Krasov anaongeza kuwa bei ya mbolea imeongezeka mara tatu (tangu 2018 hadi 2021 kwa asilimia 80) kwa sababu ya mabadiliko ya haraka ya bei ya gesi asilia (asilimia 80 za gharama kwa uzalishaji wa mbolea).

"Viwanda vingi vya kuzalisha mbolea vya Ulaya vimesitisha kazi hiyo. Hali hii inaweza kupunguza uzalishaji wa mazao ya kilimo na kusababisha uhaba wa vyakula duniani kote kwa mwaka 2023," anasema.

Krasov anasema Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, akiwa katika ziara nchini Cameroon, Julai mwaka jana, alisema mgogoro nchini Ukraine ulizorotesha tu mielekeo hasi iliyopo na iliyoathiri upatikanaji wa vyakula.

Alisema Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) linasisitiza kwamba bei za vyakula zilianza kupanda kabla ya mgogoro wa Ukraine. Kundi la watafiti la Chuo kikuu cha Kilimo cha Uswisi, lilibainisha kwamba vitendo vya Russia havihusiki na mfumuko wa bei ya nafaka.

"Wachambuzi wa Ufaransa kwa upande wao wanasema uhaba wa vyakula unasababishwa na kasoro za mfumo wa kuzalisha mazao ya kilimo duniani kote. Yaani mkazo mkubwa ulitiliwa kwa kuzalisha zao la aina moja tu, hivyo kulikuwa na upungufu wa mavuno na changamoto za kusafirisha nishati na vifaa mbalimbali," anasema.

Mtafiti Krasov aliendelea kwa kusema wataalamu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo (UNCTAD) wanatabiri kwamba kasi ya maendeleo ya uchumi wa dunia itapungua kutoka asilimia 2.5 mwaka wa 2022 hadi asilimia 2.2 mwaka huu. Hiyo ni kwa sababu ya mfumuko wa riba za kibenki, kuongezeka kwa ukali wa sheria za kodi na bajeti za nchi zilizoendelea na pia madhara ya UVIKO-19.

Anasema uchumi wa dunia unatarajiwa kuzorota na kuyumba, hasara kwa ujumla zinaweza kuwa zaidi ya Dola za Marekani trilioni 17, ambazo ni takriban asilimia 20 ya pato la dunia nzima. Pia kuna uwezekano mkubwa wa kuwapo na ukosefu wa ajira na ukosefu wa uwiano mzuri kati ya fedha za kiserikali na kibinafsi.

"Zaidi ya hayo, kuongezeka kwa idadi ya walanguzi kwenye masoko ya hisa kunasababisha kupanda kwa bei za vyakula na kupunguza uwezo wa nchi zinazoendelea kupata chakula.

Nchi za Magharibi zikiilaumu Russia kwa ukosefu wa chakula huku zinaficha ukweli kwamba wale wanaopata manufaa makubwa zaidi kutoka kuongezeko kwa bei za chakula na kuzoroteshwa kwa usafirishaji wa vyakula ni kampuni kubwa za nchi za Magharibi zinazozalisha na kuuza mazao ya kilimo," anasisitiza.

Krasov aliendelea kusema kwamba kuondoka kwa Russia katika masoko ya kimataifa ya mazao ya kilimo kunawezesha mazingira nafuu yanayosaidia kampuni za nchi za Magharibi kuendelea kunufaika.

Kwa mujibu wa Krasov, takwimu za WFP zinaonyesha kwamba bei za chakula zinaendelea kupungua ingawa Novemba, 2022 kupungua kwa bei hizo kulikuwa kidogo kulinganisha na Oktoba (asilimia 0.15). Kupungua kwa bei huko kunasababishwa na kushuka kwa bei za nafaka duniani (asilimia 1.3), maziwa (asilimia 1.2) na nyama (asilimia 0.9).

Aidha, anasema ongezeko la sasa la bei ya jumla ya sukari kwa asilimia 5.2 limesababishwa na hatua ya India kushusha kasma za usafirishaji wa bidhaa na kucheleweshwa kuingia mazao mapya. Novemba, mwaka jana, bei ya mafuta ya kula iliongezeka kwa asilimia 2.3 kwa wastani kwa sababu ya ongezeko la bei ya mafuta ya mawese na soya wakati huo huo bei ya mafuta ya mbegu kama alizeti ilipungua.

Anasema taarifa kutoka majukwaa ya biashara zinaonyesha kwamba Septemba, 2022 kulikuwa na kushuka kwa kiasi kikubwa kwa bei za mazao malighafi ya kilimo kulingana na bei kubwa zaidi zilizopatikana kutoka Machi hadi Mei, 2022 hadi kufikia bei ya mazao kadhaa kupungua kwa asilimia 40-50.

Kwa mujibu wa takwimu za Desemba 12, 2022, bei ya ngano ilipungua kutoka dola 460 kwa tani moja hadi dola 275 ilivyokuwa mwezi Mei, bei ya mafuta ya alizeti kutoka dola 2,400 kwa tani moja hadi dola 1,300 kutoka Machi na bei ya mafuta ya mbegu za rape kutoka dola 1,085 hadi dola 588 kwa tani moja Aprili.

"Hivyo bei za jumla za bidhaa za msingi za kilimo zimefikia hali ile ile iliyokuwa mwezi Novemba mwaka 2021. Na jambo hili linathibitisha kwamba vitendo vya Urusi nchini Ukraine haviathiri sana bei za vyakula duniani.

"Wataalamu wa WFP wanavyosema mbali na kupungua kwa jumla kwa bei za bidhaa tatizo la kuwa nchi zinazoendelea haziwezi kupata vyakula halijatatuliwa bado. Sababu yake ni hatua za nchi kadhaa za kupandisha gharama za kusindikiza malighafi za kilimo, kuzisafirisha na kuzifanyia bima na pia mfumko wa bei mkubwa na bei ya juu ya gesi asilia inayoongeza bei za mbolea," anasema.

Pia anabainisha kuwa Russia inaendelea kutekeleza kwa dhati dhamana zake za makubaliano ya kimataifa ya kusafirisha bidhaa za kilimo na viwanda, mbolea, nishati na zingine ambazo ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Afrika.

Mathalan, anasema mwaka 2022 Russia ilisafirisha katika soko la kimataifa nafaka takriban tani milioni 30 na kuna matumaini dhahiri kuwa inaweza kuongeza usafirishaji wa nafaka hadi tani milioni 50. Anasema hii ni dhamira njema na ya kujali maslahi ya nchi zinazohitaji sana msaada.

Anasema jambo hilo linahusika hasa na usafirishaji wa mbolea kutoka Russia kwenda nchi nyingi za Afrika, mbolea zilizo muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo barani Afrika. Anabainisha kuwa matokeo ya vikwazo dhidi ya Russia, takriban tani 280, 000 za mbolea zimezuiwa katika bandari za nchi za Ulaya.



Nafaka mbalimbali zikiwa sokoni. Kwa hivi karibuni bidhaa hizi zimekuwa zikipanda bei kutokana na sababu mbalimbali. **PICHA ZOTE MTANDAO.**



Mpunga ukiwa shambani. Uzalishaji wa mazao ya nafaka katika Afrika umeshuka kwa sababu ya ukame na sababu zinginezo.

# MAISHA

MACHI 26, 2023
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili





Ukurasa 15

## Usikubali kutumia choo kichafu



Ukurasa 14

## FUTARI YA NDIZI NAZI




## KATUNIKA

Ukurasa 16



# MWEZI WA STARA

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



1. MAJI
2. CHAI
3. SODA
4. JUISI
5. KAHAWA
6. MAZIWA

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| J | U | A | ■ | B | A | I |
| E | ■ | ■ | ■ | W | ■ | N |
| N | ■ | M | I | A | ■ | G |
| G | O | A | ■ | T | A | I |
| E | ■ | P | O | A | ■ | Z |
| W | ■ | Y | ■ | ■ | ■ | W |
| A | K | A | ■ | D | U | A |

## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU. WIKI HII NIMEWALETEA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU KUTOKA JAPAN: JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| | 3 | | |
| 4 | | | |
| | | | |
| | 2 | | |


## FUMBO TOTO

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ■ | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | ■ | | | |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


JAA, MWA, FAA, UZA, IBA, BEI, MTO, MAM, MAMBA, FUMBO, ANZISHA, MAWINGU

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI



## CHEKA



MAMA yake John alikuwa anafanya usafi chumbani kwake, ghafla alipokuwa akisafisha chini ya uvungu wa kitanda alikutana na kisanduku ndani yake kulikuwa na mawe 10.

Mama: We John kisanduku hiki cha nini?

John: Nilikuwa nayahesabu mayai ya kuku

Mama: Mayai ya kuku ndio haya mawe?

John: Hapana, mawe yalikuwa idadi ya mayai niliyoiba bandani na kuyala

Mama: Wee mtoto nitakuadhibu.

**SWALI**

Mbuga ya Taifa ya wanyama ya Nyerere ilikuwa ikitambulika kwa jina gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kwa nini mume na mke huibiana fedha?

MPENZI msomaji, leo nitajadili jambo moja ambalo limekuwa linatesa familia nyingi lakini wanaokumbana nalo hulichukulia kuwa ni la kawaida kumbe ni tatizo kubwa.

Uaminifu ndani ya ndoa zetu ni jambo la muhimu na la msingi sana. Uaminifu huu umejikita maeneo mengi na siyo tu kule kulikozoeleka eti mtu kujiheshimu asitoke nje ya ndoa. Ni kweli hilo ni eneo moja. Lakini yako maeneo mengine yanayopaswa kulindwa ili kuleta utulivu ndani ya familia.

Tabia ya udokozi au wizi imekuwa ikielekezwa zaidi kwa watoto. Wazazi wanapaswa kusimama kidete kuikemea kwa nguvu kwani ikiachwa ikue ndani ya watoto madhara yake ukubwani ni makubwa sana.

Kama tabia hizo hazikukemewa tokea awali katika makuzi yao, mara nyingi hujiimarisha hadi ukubwani. Ndio hao wengine utakuta wanaiba au wadokozi hata chakula kinapochemka jikoni. Hii ni tabia ambayo iliachwa kukemewa awali sasa imekuwa mwiba.

Kwa maneno mengine, asili ya mtu kule alikozaliwa mara nyingi ndiyo inayojitokeza pale alipo. Kile mtoto alichokiona au kusimuliwa kuhusu matendo ya wazazi wake, ndicho atakachofanya baadaye akiamini kilikuwa sahihi.

Ndiyo maana hata serikali inahimiza sana malezi na makuzi bora ya watoto kwa lengo la kuwajengea misingi mizuri ya maisha huko waendako.

Mpenzi msomaji, pamoja na ukweli huo, wako watu wanaokuwa na tabia fulani ikiwemo hiyo ya wizi na udokozi, hadi unashangaa inatoka wapi. Ndio hao nimesema kuwa huenda ni asili yao ndiyo inamtesa.

Hebu sikiliza vijana watatu wakielezea wake zao wanavyowakwapulia fedha kwenye suruali, tena wakati wakiwa usingizini.

Nikiwa kwenye daladala kiti cha nyuma kabisa, niliketi na vijana wawili. Wakati kondakta anakusanya nauli, kijana aliyekaa kulia kwangu akatoa Sh.10,000/= na zile chenji akazifurahia eti kwamba mkewe akizikuta mfukoni wakati amelala atachukua kiasi zingine atabakisha.

"Nikijisahau tu nikaacha msimbazi (Sh. 10,000), huzikwapua zote na nikiuliza asubuhi hukataa na kuniambia huenda nimemalizia kwenye pombe. Nikiweka msimbazi nyingi hukuta moja pungufu, nikiuliza anakataa.

Kijana wa pili kushoto kwangu yeye akasema: "Mimi hupenda kuwa na chenji kwani akichomoa hubakisha nikimuuliza hukubali ametoa. Tabia hii siipendi lakini nampenda mke wangu, huwa namezea tu."

Kijana wa tatu ambaye alichekesha abiria, aliposikia mazungumzo yale akadakia; Mimi hujua kuwa nimeshaibiwa pale asubuhi ninapogundua pochi imebadilishwa, badala ya kuwa mfuko wa nyuma wa suruali asubuhi naikuta mfuko wa mbele na fedha ni pungufu nikiuliza najibiwa labda umetoa kwenye pombe umesahau.

Pale walipokuwa wakitaja wake zao kuwa ni wadokozi wa hela kwenye suruali, baadhi ya kinamama waliokuwa wameketi viti vya mbele walikuwa wakigeuka nyuma na kuwashangaa bila kusema neno.

Mimi nilikuwa nawachokonoa wazidi kuongea kwa sababu nilikuwa natafuta cha kuchombeza kwenye safu hii. Si unajua Maisha Ndivyo Yalivyo?

Nikahojiana na watu wengine kadhaa, mmoja akasema baada ya kugundua anaibiwa kiaina na mkewe, huwa analala usingizi wa mang'amung'amu (wasiwasi) ili amnase lakini wapi.

Mwishoni akaona ujinga akawa anajilalia fofofo. Nikawauliza labda hamtoi matumizi ya kutosha nyumbani wakajibu siyo hivyo, labda ni tabia tu ya wake zetu.

Naam. Sikia kituko kingine. Wakati nikiwa katika saluni moja, kijana mmoja akaeleza kisa kilichotokea usiku nyumba aliyopanga. Kilikuwa kinafanana na mazungumzo ya hapo juu niliyosikia ndani ya basi.

Ila maelezo yake ni kwamba badala ya mama kusolomoa fedha mfukoni mwa mumewe, mwanaume ndiye aliyechomoa fedha kwenye pochi ya mkewe.

Maelezo yakawa namna hii: Iko familia moja ambayo imefunga ndoa yapata miaka miwili sasa na bado hawajabahatika kupata mtoto. Ni ndoa iliyojaa vitimbwi sana. Hivi majuzi ndiyo zogo likatibuka pale mke aliporejea kutoka msibani akakuta mumewe kachomoa fedha pale alipokuwa amezificha na kwenda kujinafasi na kimada.

Msiba ule ulimhusu pia mume huyu lakini alipojua kuwa mkewe lazima alale huko, yeye alirejea nyumbani na kusaka fedha za mkewe kila mahala na alipozikuta akaishia kwa kimada wake.

***Mke aliporejea kuangalia fedha zake hajazikuta na alipomuuliza mumewe akakataa kuzichukua. Watu mko wawili ndani ya nyumba au chumba ni chenu bado uaminifu hakuna. Maisha ndivyo yalivyo. Je, una kisa? Ujumbe 07268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Kwenye afya ndiko tunakouona ufukara usiopakwa rangi

NI mwendawazimu peke yake anayeweza kuamini kwamba anaweza kuitelekeza afya yake kwa matarajio kwamba dola au jamii, au mtu mwingine atajali na kuishughulikia.

Aidha, ni mwendawazimu huyo huyo anayeweza kufikiri kwamba kila mtu akijali afya yake binafsi, tutakuwa tumemaliza matatizo ya afya ya jamii. La hasha! Iko nguvu ya umma inahitajika.

Nataka kusema nini? Waraka wa Ndani, leo umejikita kufuta mtazamo hasi wa baadhi ya watu kusita au kupuuza suala la kuchunguza afya zao na hasa ugonjwa wa kifua kikuu, unaosababishwa na bakteria maarufu 'mycobacteria tuberculosis.'

Ugonjwa huu huathiri mapafu, mishipa ya fahamu, mifupa, mfumo wa mzunguko wa damu, ngozi, viunganishi vya mifupa na 'lymphatic system'. Virusi hivyo viligunduliwa na Mwanasayansi wa Ujerumani, Robert Koch, mwaka 1882.

Nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ya Machi 24, mwaka huu, aliyesema kila mmoja wetu ana wajibu wa kuhakikisha anachukua hatua zote za tahadhari katika mapambano dhidi ya kifua kikuu ili kukata mnyororo wa maambukizi mapya na kuzuia vifo visivyo vya lazima.

Katika hotuba yake, amenukuliwa akisema, mgonjwa mmoja wa kifua kikuu ambaye hajagunduliwa, ana uwezo wa kuambukiza watu zaidi ya 10 hadi 20 kwa mwaka. Tunajua Tanzania na dunia kwa ujumla, zimejikita kutokomeza ugonjwa huu ifikapo mwaka 2030.

Kanzidata ya taifa inaonyesha idadi kubwa ya waathirika wa ugonjwa huu wanaogunduliwa katika miaka ya usoni ni wachimbaji wa madini, ambao kutokana na uchimbaji usiozingatia njia sahihi za kujikinga na vumbi litokanalo na upasuaji, uchorongaji na usafirishaji wa udongo au mchanga wenye madini, ndio wahanga wakuu wa TB.

Yako pia makazi duni, ambayo hujengwa na walio wengi vijijini. Hujenga nyumba zisizo na madirisha makubwa ya kupitisha hewa ya kutosha lakini pia msongamano wa watu nao huathiri na kuchochea maambukizi ya ugonjwa huu hatari na unaoua wengi. Kwa Tanzania, takwimu zinaonyesha kuwa kila siku watu 71 hupoteza maisha kutokana na ugonjwa huu.

> **Nataka kusema nini? Waraka wa Ndani, leo umejikita kufuta mtazamo hasi wa baadhi ya watu kusita au kupuuza suala la kuchunguza afya zao na hasa ugonjwa wa kifua kikuu, unaosababishwa na bakteria maarufu 'mycobacteria tuberculosis.'**

Katika hali hiyo, ni dhahiri kwamba tunahitaji nguvu ya pamoja, kwa maana ya utashi wa umma wenyewe katika kuinua kiwango cha elimu na uelewa wa kutosha wa wananchi wake kuhusu masuala ya siha ya umma wa Watanzania na kuwekeza zaidi katika jitihada za makusudi.

Ni lazima sasa tuwe na kampeni za kudumu za kuwahamasisha Watanzania na kuwakumbusha kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi wa afya zao kila mara. Ngoja niwaambie ukweli pasina shaka, kwamba bado hatujawekeza ipasavyo katika siha yetu kama taifa.

Kwa mfano, takwimu zinaonyesha kwamba tumepunguza maambukizi mapya ya kifua kikuu kutoka wagonjwa 306 katika kila idadi ya watu 100,000 na kufikia wagonjwa 208 katika kila watu 100,000 ikiwa ni sawa na kupungua kwa asilimia 32.

Katika Hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto, kanzidata inaonyesha kuwa asilimia 70 ya wagonjwa wanaolazwa wodi moja katika hospitali hiyo wanatumia hewa tiba ya Oksijeni. Kwamba huduma hiyo wodini inawahusisha wagonjwa kati ya 20 hadi 30, ambapo gharama kwa mtungi mmoja wa Oksijeni kwa sasa ni zaidi ya Sh. 45,000.

Iko haja ya kuanzisha kampeni ya kitaifa kama tunavyoweka nguvu kubwa hivi sasa katika kutoa elimu kuhusu mlipuko wa ugongwa wa 'Marburg' ulioua watu sita na wengine watatu kulazwa huko mkoani Kagera. Watanzania wapewe elimu bila kujali gharama, lasivyo, tutapoteza idadi kubwa ya watu wetu.

Ziko tafrisi nyingi, lakini mojawapo ni kwamba idadi kubwa ya Watanzania, hasa walioko vijijini na pembezoni hawajafikiwa na elimu ya kutosha kuhusu ugonjwa huu TB. Wengi wanaoishi huko, ndiko tunakoona ufukara kwa uhalisia, usiopakwa rangi. Huko ndiko waliko wazalishaji wakuu wa pato la taifa.

***Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.***
***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com***
***Simu ya mkononi: +255 767 535490***









Watu wengi hawapendi kuvaa nguo za harusi zikiwa za rangi nyekundu kutokana na imani tofauti, lakini vazi la rangi hiyo linapendeza zaidi kuvaliwa katika siku hiyo muhimu. Pichani ni baadhi ya nguo za rangi nyekundu zilizovaliwa na maharusi.

## MITINDO



# MWEZI WA STARA

MWEZI mtukufu wa ramadhani umeanza, kuna mambo mengi ya kuzingatiwa katika kutimiza nguzo hiyo muhimu kwa Waislamu.

Moja ya vitu muhimu vinavyozingatiwa kwa wanawake na wanaume ni kuvaa mavazi ya stara yanayohifadhi kiasi kikubwa cha mwili.

Kwa sasa ukitembea mjini utakuta wanawake wengi wamevalia mabaibui au magauni marefu yaliyofunika mwili wao huku wanaume wengi wakiwa wamevalia kanzu.

Hata hivyo mavazi hayo ya stara wanayovaa wanawake huwapendeza, hivyo wanatamani wangekuwa wakiyavaa wakati wote si tu katika mwezi huu mtukufu.

Hata hivyo, stara inampa mwanamke heshima, kujiamini, kuwa na mvuto na kumfanya apendeze zaidi.

Hata kwa wanawake ambao si Waislamu hununua mavazi ya stara na kuyavaa katika kipindi cha Mwezi huu.

UREMBO

Na Mary Geofrey



# KUCHA BILA FANGASI

FANGASI za kuch[a] ni [illegible] wanawake, na kwa wanaume huwaathiri hasa kwenye kucha za miguuni.

Fangasi hizi husababisha kupoteza mvuto wa kucha za mikononi na miguuni kwa sababu zinakuwa zinabadilika rangi kuwa nyeusi au rangi ya kuvimbia usaha.

Katika safu hii tutaelekezana namna ya kuepuka kupata maambukizi ya fangasi lakini pia namna ya kuzitibu ukiwa nyumbani kwako.

**Njia za kuzuia fangasi**

Kuosha mikono yako baada ya kushika kucha iliyoathirika, kausha vidole vizuri baada ya kuoga hasa eneo la katikati ya vidole vya miguu.

Aidha, pata huduma za manicure na pedicure kutoka kwenye saluni ya kuaminika na epuka kutembea peku kwenye maeneo ya watu wengi.

Punguza matumizi ya kucha za bandia na rangi za kupaka kucha.

**Namna ya kutibu fangasi**

**Mafuta ya mti wa mchai**

Mafuta haya yana viambata vya kupambana na fangasi pamoja na vimelea wabaya. Matumizi yake ni kwa kupaka kwenye kucha mara mbili kwa siku kwa kutumia pamba.

**Apple cider vinegar:**

Chukua vijiko vitano vya apple vinegar, changanya na maji nusu lita, kisha chovya mguu ulioathirika kwa dakika 20 kila siku.

**Kitunguu saumu:**

Unaweza kutibu fangasi ya kucha kwa kutumia kitunguu saumu kwa kuponda kitunguu chako na kupakaa eneo la kucha, kisha subiri kwa dakika 30 ndipo jisafishe.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# FUTARI YA NDIZI NAZI



MWEZI mtukufu wa ramadhani umeanza huku changamoto kubwa kwa wanawake ni kukimbizana na muda wa kuwahi kupika futari.

Katika safu hii leo tutaelekezana aina za futari ambazo hazichukui muda mrefu kupika ili familia iwahi kufuturu.

Katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuna changamoto ya muda kwa wafanyakazi hususani wanawake.

**Futari ya ndizi mbivu**

Mahitaji ni ndizi mbivu sita, nazi pakiti moja, sukari kiasi na hiliki ya kutosha.

**Namna ya kupika**

Menya ndizi kisha toa moyo wa katikati, zikatekate kulingana na unavyotaka, zipange ndani ya sufuria.

Weka maji kiasi kulingana na wingi na ugumu wa ndizi, zichemke kidogo zikikaribia kuiva na kabla maji hayajakauka kabisa weka tui la nazi, mimina hiliki na sukari ziache zichemke hadi tui libaki kidogo, zitakuwa tayari kwa kuliwa.

Unaweza kula futari yako na uji, chai, maziwa na kushiba kabisa kusubiri mlo wa daku.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Usikubali kutumia choo kichafu

USAFI wa nyumba wa mara kwa mara ni nguzo kubwa ya kuistawisha na kuipendezesha. Isipofanyiwa usafi wa uhakika huchakaa mapema na hata kuharibika kabisa.

Lakini leo nitapenda kuzungumza baadhi ya dondoo za namna ya kusafisha sehemu za bafu na choo.

Kabla ya kuanza kusafisha bafuni, kwanza ondoa vitu vyote vya kuhamishika, wakati huo huo ukihakikisha dirisha liko wazi ili hewa ipite na kuondoa hewa nzito iliyoko katika bafu na choo.

Baada ya hapo ondoa buibui kwenye kona zote za dari ikifuatiwa na kufuta vumbi mlangoni na sehemu za ndani na nje.

Wakati wa kusafisha, ni vyema kuanzia juu kushuka chini ili kuruhusu taka za vumbi na buibui zimwagike sakafuni kwa ajili ya kusafisha mwishoni

Ukishafanya hivyo, weka dawa ya kusafishia katika sehemu zenye uchafu ili iwe rahisi wakati unasugua.

Ni vyema ukazingatia maelekezo ya dawa ya kusafishia ili kuwa na uhakika unatumia kiasi sahihi ambacho hakiwezi kuharibu.

Katika kuta za bafu pia unapaswa kupaka sabuni au dawa zingine za kusafishia endapo zitakuwa za marumaru na kwa kutumia sponji au brashi. Unaweza kusugua sehemu uliyoweka sabuni hiyo huku ukihakikisha unaisuuza kuondoa michirizi yote ya uchafu. Kama ukuta ni wa karibu na sinki au bakuli la choo, ukaushe kwa taulo.

Ni muhimu kukumbuka kuvaa glovu wakati wa kusugua kwa kuwa baadhi ya dawa na sabuni zinaweza kuwa na kemikali kali, hivyo kusababisha kuchubua ngozi. Safisha kioo kwa kutumia maji na taulo au dawa ya kusafishia vioo na taulo.

Safisha nje ya choo ukianza na sehemu ya juu ya kuvuta maji, kwa taratibu unaweza kuendelea kusafisha eneo lote la nje ya choo ambalo ni pamoja na mfuniko na eneo la chini ya sehemu ya kukalia na kupafuta na taulo.

Kwa upande wa sakafu, hakikisha usafi wako unaanzia sehemu zilizojificha hadi zile za wazi. Ni vyema kusafisha vumbi na uchafu wote ulio chini eneo la choo lilipounganika na sakafu.



## Aina 10 za maua ya kusafisha hewa ndani



WIKI iliyopita tulikueleza aina ya maua ambayo yanafanyakazi mahsusi ya kusafisha hewa ndani ya nyumba. Katika Makala hiyo, tulikutajia ua moja tu miongoni mwa 10 yanayosifika kwa kazi hiyo.

Katika makala ya leo, tunakutajia aina tisa za maua hayo ambayo kiuhalisia ni rahisi kuyapata, kuyatunza na kazi yake kwenye nyumba ni kubwa sana.

Kwenye orodha ya wataalam wa mimea na maua, baada ya 'snake plant' ni HYPERLINK "https://amzn.to/2KC7lnI" \t "_blank" Lucky Bamboo, HYPERLINK "https://rstyle.me/n/dfu2c3cdwj7" \t "_blank" Spider Plant, HYPERLINK "https://rstyle.me/n/dfu2hacdwj7" \t "_blank" ZZ Plant, HYPERLINK "https://rstyle.me/+V21I1CvKR8kP-otOLBjg1g" \t "_blank" Golden Pothos, Boston Fern, HYPERLINK "https://rstyle.me/n/dfvnff-cdwj7" \t "_blank" Red Prayer Plant, HYPERLINK "https://rstyle.me/+eiiSNWt0Vw7rnRFkNZSeEA" \t "_blank" The Areca Palm, HYPERLINK "https://rstyle.me/n/dfu2fhcdwj7" \t "_blank" Peace Lilly, HYPERLINK "https://amzn.to/2yRjRfL" \t "_blank" Peperomia na Money Plant.

Orodha hii ya maua ina sifa zinazofanana kwa maana ya kwamba kazi yake kubwa ni uwezo wake wa kusafisha hewa kwa kuongeza kiwango kikubwa cha oksijeni.

Kadhalika, ni maua ambayo ni rahisi kuyatunza. Hayahitaji viuatilifu vingi, maji mengi wala mbolea nyingi.


Maua haya yanahitaji mwanga mdogo, maji kidogo sana (unaweza kumwagilia mara moja kwa wiki), mbolea kidogo na hayahitaji madawa ya kuua wadudu kwa kuwa hayashambuliwi sana.

Wataalam wanaeleza kuwa kwa wapenzi wa maua wasiwe na 'wazimu' wa kununua kila ua badala yake wazingatie aina hii ya maua ili kuboresha hali ya hewa ya nyumbani.

# KATUNI


## KATUNIKA KI'DOMOKRASIA

BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766




JUKWAANI













*KINYUNYIZO CHA LEO...

MAISHA HAYAPIMWI KWA KUISHI UKWENI...

## Russia yapoteza wanajeshi 30,000 mji wa Bakhmut

IMEELEZWA vita vinavyoendelea katika mji wa Bakhmut, nchini Ukraine, imepoteza au kujeruhi wanajeshi kati ya 20,000 na 30,000 wa Russia.

Kamanda mkuu wa Ukraine, alisema hali imekuwa tulivu kwa siku mbili baada ya mapigano makali kutulia.

Mapema mwezi huu, maofisa wa Magharibi walikadiria Russia kupoteza wanajeshi hao tangu msimu uliopita wa joto.

Kamanda huyo, Valerii Zaluzhnyi alisema juhudi kubwa za wanajeshi wa Ukraine zinawarudisha nyuma vikosi vya Russia.

Russia ina matumaini ya ushindi baada ya kushindwa kupata mafanikio makubwa katika siku za hivi karibuni.

Licha ya hayo, wachambuzi wa masuala ya kijeshi wanaamini kuwa Bakhmut ina thamani ndogo ya kimkakati, na umuhimu wa jiji hilo kibiashara.

Katika mtandao wa Facebook, Luteni Jenerali Zaluzhnyi alisema kwamba wakati hali kwenye mstari wa mbele ni ngumu zaidi katika mwelekeo wa Bakhmut, lakini juhudi za vikosi vya ulinzi, watafanikiwa kuleta utulivu.

Luteni Jenerali Zaluzhnyi alichapisha ujumbe huo baada ya kuzungumza na Mkuu wa Majeshi wa Uingereza, Admirali Sir Tony Radakin, kuhusu hali ya Ukraine.

Maoni yake ni ishara chanya ya hivi punde kutoka kwa maofisa wa Ukraine kuhusu vita virefu vya Bakhmut.

Alhamisi, Oleksandr Syrsky, kamanda wa vikosi vya ardhini vya nchi hiyo, alisema kuwa wanajeshi wa Russia wamechoka huko Bakhmut.

Syrsky aliongeza kuwa Russia haijakata tamaa ya kuchukua Bakhmut kwa gharama yoyote licha ya kupata hasara ya wanajeshi wake na vifaa.

Mji huo ulikuwa na wakazi 70,000 kabla ya kuanza kwa vita lakini sasa umesalia na watu wachache, wengi wakikimbia kunusuru maisha yao.

**BBC**

## Rwanda yamuachia huru Rusesabagina

**KIGALI,** RWANDA

PAUL Rusesabagina ambaye alikuwa akitumikia kifungo jela kwa madai ya kuikosoa serikali ya Rwanda, ameachiliwa huru juzi usiku.

Raia huyo wa Ubelgiji mwenye asili ya Rwanda, na mkazi wa kudumu wa Marekani baada ya kuachiliwa kutoka gerezani alikwenda moja kwa moja hadi kwenye makazi ya balozi wa Qatar mjini Kigali kuomba hifadhi.

Kulingana na ofisa wa Marekani, huenda akabaki kwenye makazi hayo kwa siku kadhaa kabla ya kwenda nchini Qatar, ambayo ilisaidia mchakato wa kuachiliwa kwake.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Anthony Blinken, alitoa taarifa ya kukaribisha hatua hiyo ya kuachiliwa kwa Rusesabagina, ingawa maofisa wa nchi hiyo walisema hakukua na ahadi yoyote ambayo wangeitoa kwa Kigali zaidi ya kuitambua hatua hiyo hadharani.

"Ni faraja kujua kwamba Paul anaungana na familia yake na serikali ya Marekani inaishukuru serikali ya Rwanda kwa kufanikisha kuwaunganisha," alisema Blinken.

Pia aliishukuru serikali ya Qatar kwa msaada wao utamwezesha Paul kurejea Marekani.

Rusesabagina, shujaa wa filamu ya Hotel Rwanda aliyesifika kwa kuokoa maisha ya watu 1,200 katika hoteli aliyoisimamia wakati wa HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/wiki-ya-kumbukumbu-ya-mauwaji-ya-kimbari-nchini-rwanda/a-61396867" mauaji ya kimbari ya 1994 alikuwa mkosoaji wa Rais Paul Kagame na alihukumiwa kifungo cha miaka 25 jela kwa tuhuma za ugaidi.

**BBC**

# Marekani, China zavutana mradi kuunganisha dunia

**WASHINGTON**, MAREKANI

USAMBAZAJI wa nyaya za chini ya bahari, ambazo hubeba data za ulimwengu, zimeleta vita vya teknolojia kati ya Marekani na China.

Marekani inayohofia mradi huo kutumiwa na majasusi wa China, imezuia miradi kutumiwa na raia wa nchi hiyo wanaoishi nje.

Pia iliziba njia za waya za kampuni ya Big Tech kuingia Hong Kong.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, vita hiyo ilianza kibiashara katika mkataba mkubwa wa kibinafsi wa kupitisha nyaya za mtandao chini ya bahari.

Ilizua uhasama katika vita vya wakala kutoka Marekani na China juu ya teknolojia hiyo ambayo inaweza kuamua ni nani atakayetawala kiuchumi na kijeshi katika miongo kadhaa ijayo.

Februari mwaka huu, kampuni ya usambazaji nyaya za chini ya bahari ya Marekani ya SubCom LLC ilianza kuweka nyaya katika mradi huo wa thamani ya dola milioni 600, ili kusafirisha data kutoka Asia hadi Ulaya, kupitia Afrika na Mashariki ya Kati, kwa zaidi ya maili 12,000 za nyuzinyuzi zinazopita kwenye sakafu ya bahari.

Mradi huo unaojulikana kama South East Asia-Middle East-Western Europe, utaunganisha nchi kumi na mbili huku ikitokea Singapore hadi Ufaransa, ikivuka bahari tatu. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mnamo 2025, ukiwa ni mradi ambao uliteleza kupitia vidole vya China.

China ndiyo ilikuwa iutekeleze kupitia kampuni yake ya HMN Technologies Co Ltd, lakini ilielezwa Marekani iliingilia kati ikihofia ujasusi unaowezwa kufanywa na China.

**BBC**



Mkurugenzi Mtendaji wa TikTok, Shou Zi Chew, akijiandaa kutoa ushahidi mbele ya Kamati ya Nishati na Biashara ya Bunge la Marekani, katika Jengo la Capitol Hill juzi. **PICHA: AFP**

## Wahamiaji 34 wahofiwa kufa maji

**TUNIS,** TUNISIA

WAHAMIAJI 34 kutoka nchi za kusini mwa jangwa la Sahara, wanahofiwa kuzama maji katika pwani ya Tunisia baada ya boti walilokuwa wakisafiria kupinduka.

Tukio hilo ni la tano kutokea eneo hilo likiwahusisha wahamiaji kuzama ndani ya siku mbili, huku watu saba wakithibitishwa kufariki dunia hadi jana.

Kulingana na taarifa kutoka vyombo vya kuaminika, watu wengine 67 bado hawajulikani waliko.

Walinzi wa pwani ya Tunisia, waliripotiwa kusimamisha boti 56 kuondoka nchini humo kuelekea Italia, katika siku mbili zilizopita.

Houssem Jebabli, kutoka kwa Walinzi wa Kitaifa wa Tunisia, alisema kuwa zaidi ya wahamiaji 3,000 wamezuiliwa wakitaka kujaribu kuondoka nchini humo.

Tunisia imekuwa kitovu cha kuondokea wahamiaji kuelekea Ulaya. Takwimu za Umoja wa Mataifa zinaonyesha kuwa takriban wahamiaji 12,000 waliowasili nchini Italia mwaka huu, walitokea Tunisia, ikilinganishwa na 1,300 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Mwezi uliopita, Rais wa Tunisia Kais Saied, aliwashutumu wahamiaji kutoka nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara wanaoishi nchini humo kwa kusababisha wimbi la uhalifu na kuwataja kuwa ni tishio la idadi ya watu.

Maoni yake yalishutumiwa vikali na Umoja wa Afrika huku mashirika ya haki za binadamu yakiikosoa hotuba yake kwa kusema ni hotuba ya chuki na ya kibaguzi.

**BBC**

MAKALA

# KAULI YA MWALIMU NYERERE IMETIMIA



Na Magabilo Masambu

MWAKA 1962, Rais wa kwanza wa Tanganyika na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliandika kijitabu kinaitwa "Tujisahihishe". Kijitabu hiki kimekuwa maarufu sana kwa sababu kimekuwa kikitajwatajwa sana kama rejea katika siasa za nchi yetu. Umaarufu wake unatokana na maarifa makubwa yaliyoandikwa kwa ustadi mkubwa uliojaa hekima nyingi.

Katika ukurasa wa tatu, Mwalimu alisema maneno yafuatayo: "Ni kweli kwamba demokrasia haiwezi kudumu ikiwa wachache hawatakubali matakwa ya wengi, lakini matakwa ya wengi hujulikana katika majadiliano au mazungumzo ya wazi wazi.

"Kadhalika, matakwa ya wachache hujulikana katika majadiliano na mazungumzo. Bila wale wachache kusema waziwazi matakwa yao, majadiliano hayana maana. Wakati mwingine hata baada ya majadiliano, wachache japo wamekubali kutii uamuzi wa wengi bado wanaweza kuendelea kuamini kwamba, mawazo yao ni sahihi na ya walio wengi yamepotoka.

"Demokrasia inawapa haki na ukweli unawapa wajibu wa kuendeleza mawazo yao mpaka wengi waone kuwa ni ya kweli. Bila hivyo maendeleo katika mawazo hayawezekani, kwani mara nyingi wazo zuri hutokana na mtu mmoja tu. Mwanzo laweza likapingwa, pengine kwa nguvu kabisa na walio wengi, lakini hatimaye wengi hulikubali. Huu ndiyo msingi wa maendeleo katika mawazo ya binadamu."

Sasa, Machi 8, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi katika shughuli iliyoandaliwa na Baraza la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA) kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ambayo imekuwa ikifanyika kila ifikapo Machi 8 kila mwaka.

Jambo hili liliibua mijadala mingi pengine ndani na nje ya nchi. Hii ni kwa sababu kwa kipindi cha uongozi wa awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli, palikuwapo na sintofahamu kati ya serikali inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na vyama vya siasa vya upinzani. Chuki za waziwazi zilionekana kati yao huku mazingira ya ufanyaji wa shughuli za kisiasa yakiwa magumu kwa vyama hivyo. Hatua hiyo ilisababisha serikali ya sasa chini ya Rais Samia kufanya majadiliano na mazungumzo ya kuleta umoja kati ya serikali na vyama vingine vya siasa.

Kama ambavyo Nyerere amesema wazo zuri hutoka kwa mtu mmoja tu, nataka niamini kwamba safari ya majadiliano na mazungumzo haya yaliyoleta ushirikiano baina ya serikali na vyama vya upinzani, kwa vyovyote vile, wazo hilo lilitoka kwa mtu mmoja tu ambaye sjui ni nani. Anaweza kuwa Rais Samia mwenyewe au mwingine aliyesema: "Jamani nadhani turidhiane na hawa watu, hakuna namna tunaweza kuongoza chini peke yetu" na hapo mazungumzo yakaanza na kweli tuliona majadiliano yalikuwa yanafanyika waziwazi maana kila walipotoka kwenye majadiliano waliujulisha umma kinachoendelea.

Ukisikiliza hotuba ya Rais Samia pamoja na ya Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA siku ya maadhimisho ya BAWACHA, utagundua kwamba jambo hili halikuwa raihisi. Haikuwa rahisi kwa wanachama wa CCM wala CHADEMA na kwa sababu hiyo, naamini maneno ya Mwalimu Nyerere kwamba jambo likitoka kwa wachache linaweza kupingwa na wengi lakini baadaye linaweza kueleweka baada ya hawa wachache kusema waziwazi matakwa yao mpaka wale wengi watakapoelewa.

Upande wa pili, wanachama wa vyama vya upinzani ambao wanaonekana ni wachache kwa mtazamo, pamoja na uchache wao, wameendelea kuwaeleza walio wengi kutoka CCM mpaka walipokubali na kuona kwamba hawa wachache wanayo mambo ya msingi na kukubali kuketi pamoja kwa mazungumzo.

Binafsi, niwapongeze sana viongozi wa pande zote waliokubali kufanya majadiliano na kufikia mwafaka wa kuanza kushirikiana. Hili ni jambo jema na lenye afya kwa nchi. Hakuna sababu ya kugombana kwa misingi ya vyama vya siasa. Kama tumeishi miaka yote tukishirikiana bila kujali dini, rangi, makabila yetu yaani shughuli ya Mwislam ni yetu sote, shughuli ya Mkristo ni yetu sote, Mkurya, Mjita, Msukuma, Mkwere na kadhalika tunajumuika pamoja, kwa nini vyama vya siasa?

Serikali inatoza kodi bila kuangalia dini, kabila au chama. Sasa kwa nini linapokuja suala la madaraka na uongozi inakuwa taabu? Kwa hiyo kwanza nimpongeze mwasisi wa jambo hili la maridhiano, najua si rahisi kueleweka kwa wote kwa haraka lakini jambo zuri huwa halitoki kwa wengi bali wengi huhitaji kushawishiwa kwa hoja mpaka watakapokubali kwa kuelewa maana halisi ya jambo lenyewe.

Ni imani yangu kwamba ushirikiano huu utazaa utaratibu mzuri wa kisheria (Katiba) ili makubaliano na ushirika huu ulindwe kwa mujibu wa sheria na si kwa mujibu wa mtazamo wa mtu maana mtu huyo akiondoka, tunaweza kurudi tena kwenye uhasama maana hatujui atakayekuja atakuwa anaamini katika nini.

Migogoro mingi ya kidunia na hata katika jamii zetu, inatokana na utamaduni wa kukwepa majadiliano na mazungumzo. Hata vita tunavyovisikia au mazungumzo hayajafanyika au hayakuleta matunda, lakini tukijenga utamaduni wa kufanya mazungumzo pale panapotokea migogoro, hatutakuwa tunafikia kuumizana. Ni kweli kwamba migogoro ni sehemu ya maisha na maisha hayawezi kukamilika bila migogoro kwa sababu inatokana na utofauti tulionao katika kufikiri lakini pamoja na tofauti za kimtazamo, tunaweza kuwa na Amani na upendo miongoni mwetu na kuepusha shari na migogoro miongoni mwetu.

Kwa ushauri wangu, baadhi ya wanachama wa vyama vya upinzani wanawatuhumu viongozi wao kwamba wamelambishwa asali, lakini pia baadhi ya wanachama wa CCM bado hawajamuelewa mwenyekiti wao, Rais Samia. Wakati Nelson Mandela anatoka gerezani baada ya miaka 27 ya kifungo akawa Rais wa Afrika kusini, alipofanya kazi na sehemu ya wale waliomfunga watu hawakumwelewa. Kwa kufanya hivyo, pengine kwa msemo wa sasa, tungesema alilambishwa asali lakini tumeona baadaye walikuja kuelewa.

Kwa hiyo basi, pande zote mbili kama mmeweza kuwaamini viongozi wenu kwa muda mrefu, aminini hata haya wanayoyafanya yana nia njema kwa taifa. Mataifa makubwa duniani yanaungana kufanya kazi pamoja sisi vinchi vidogo tunaleta migogoro ya wenyewe kwa wenyewe. Hakuna sababu, tuungane tushirikiane tuijenge Tanzania kwa manufaa ya wote.

Hapa tulipofika tunahitaji kufanya zaidi, ili waliokuwa wameshapoteza imani na sisi warudi kutuamini, kwani sisi ndio tulioongoza harakati za ukombozi hasa kusini mwa Afrika. Tusipofanya hivyo tutafanana na watu wanaopenda sana kutoa misaada kwa marafiki na jamaa ili kutafuta sifa za kijinga huku wakishindwa kuzisaidia familia zao.

Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR-ES-SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mgonjwa aliyemuagiza mwenzake kumsaka mpenzi wake aliyemtelekeza hospitalini



Na Adam Fungamwango

UNAJUA mwenzangu karibuni utatoka hospitalini, utokapo tafadhali, fika mjini umtafute mpaka umuone, mchumba wangu Clara."

Ukiyasoma maneno haya utagundua tu kuwa anayeongea hapa ni mgonjwa, tena mgonjwa aliyelazwa hospitalini, anayejaribu kumwagiza mgonjwa mwenzake anayeonekana kuwa nafuu kuliko yeye na tayari madaktari wameshamthibitishia kuwa atatoka hivi karibuni.

Mgonjwa ambaye bado hana mategemeo ya kutoka kutokana na maradhi yanayomkabili anamwambia mwenzake kama akijaliwa kutoka, afike hadi mjini na kumtafuta mchumba wake, Clara. Inaonekana mgonjwa huyo ni mpweke na tangu alazwe hajamwona mpenzi wake. Inawezekana ndugu zake wote walifika kumwona lakini roho yake haijatulia na hatotulia mpaka atakapomuona Clara.

Maneno haya niliyoanza nayo yapo kwenye wimbo unaoitwa 'Clara', uliofyatuliwa na DDC Mlimani Park Orchestra katikati ya miaka ya 1980, ukitungwa na Maximillian Bushoke. Hebu tuendelee kusikiliza mgonjwa akiendelea kumwagiza mgonjwa mwenzake, wote wakiwa kitandani, wakiugulia kwa maumivu.

"Nyumbani anakoishi ni Msimbazi Kota, ukimwona mpe salamu nyingi sana mueleze mchumba wako Kitwana anakusalimu.

Kama hajasikia eee, kama hajasikia, eee, ajali iliyonipata nimekuwa kilemaa, na kilema isiwe kisingizio cha kukosa kuja kuniona."

Hapa sasa tunalifahamu jina la mgonjwa anayemwagiza mwenzake kuwa ni Kitwana na pia amelazwa kutokana na kupata ajali, amekuwa mlemavu. Anamwambia mwenzake kuwa nyumbani kwa mpenzi wake ni Msimbazi Kota, akishamtafuta na kumwona, ampe salamu nyingi sana, halafu amweleze mchumba wake Kitwana anamsalimu.

Na kama hajapata taarifa ni kwamba mpenzi wake huyo amepata ajali na sasa amekuwa kilema, lakini ulemavu alio nao si kisingizio cha kwenda kumwona.

Ina maana bado Kitwana hana uhakika kama mchumba wake huyo amesikia hizo habari za ajali iliyompata. Pia akamsisitizia kama aliipata, halafu hakwenda kwa sababu amesikia ameshakuwa mlemavu, basi hajafanya vyema kwa sababu ulemavu si kisingizio cha kutofika kumwona.

"Tafadhali, ukimwona muulize kama kweli Clara yuko radhi niteseke hospitalini. Kwa maradhi bila kunijulia hali, kwa maradhi bila kunijulia hali."

Kitwana anaendelea kama kulalamika hivi kuwa akimwona amwulize kama amepata hizo taarifa na kama akizipata basi aende hospitalini haraka akamwone mpenzi wake. Na kama alizipata lakini amepotezea, je ni kweli imefika wakati Clara yuko radhi kumwona akiteseka hospitalini kwa maradhi bila kwenda kumjulia japo hali?"

Ni mashairi ya masikitiko kwenye wimbo unaoonyesha baadhi ya matatizo yanayowapata watu kwenye jamii. Kuna wapenzi au hata wanandoa wanapendana wakati wakiwa na afya njema lakini mmoja akishakuwa mgonjwa, basi inakuwa matatizo.

Nilisema ugonjwa si ule wa siku mbili tatu, la hasha. Kuna magonjwa ambayo yanampata mwanadamu lakini yanachukua muda mrefu kupona na mengine yanakuwa ya kudumu, ikiwemo ulemavu. Hapa ndipo kwenye matatizo.

Wake wameshawakimbia waume zao na kuwaacha hospitalini wakiteseka au vitandani majumbani baada ya kuona sasa kwao itakuwa mzigo. Lakini awali alikuwa akihudumiwa akipata chochote anachokitaka, mwezake amepata mtihani anashindwa kukumbuka wema aliofanyiwa na kukiuka hata kiapo cha ndoa kwa wale waliofunga ndoa.

Na wanaume nao wapo waliowatelekeza wake zao baada ya kuona hawawezi kuwapa chochote wanachohitaji kwa sababu ni wagonjwa.

Watawachukua na kuwarudisha kwa wazazi wao wakijifanya akae hapo ili awe anapata huduma nzuri kwa sababu ni kwao, lakini akiondoka hapeleki mahitaji yoyote, badala yake ataendelea kula raha na wanawake wengine.

Mwingine anaona aibu kumtimua, au kumpeleka kwao, badala yake anamtelekeza na kwenda kuishi na mwanamke mwingine, huku akiwa anamuacha mwenzake na ugonjwa na majonzi juu.

Hii si tabia nzuri kibinadamu hata kwa wale ambao ni wapenzi tu wa kawaida au wachumba kwa sababu wakati mwingine hiyo ni mitihani tu, baadaye mwenzako anapona na unabaki na aibu, unashindwa kwenda kumuomba hata msamaha huku ukiwa unampenda, ila ulikimbia majukumu.

Kwa wanandoa ni mbaya zaidi kwa sababu kwenye dini zote, wakati wa kufunga ndoa mke na mume huulizwa kama wataishi kwa shida na raha na kila mtu alikubali. Kwa raha mmeishi, lakini mbona kwenye shida hali inabadilika? Kwa msingesema siku ile ya ndoa kuwa kwenye shida hapana? Mlikuwa mnadanganya? Na mlikuwa mnamdanganya nani?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

MIEZI miwili tu baada ya ndoa, Husna anapigiwa simu ya mtu asiyemfahamu. Haikuwa simu ya heri. Ni simu ya mtu anayeonekana amedhamiria. Amedhamiria kufanya kitu alichokikusudia. Kwenye maisha ya ndoa aliambiwa yatakuwa ya shida na raha, lakini kwake haikuwa mapema kiasi hicho. Alihisi sasa hakuingia kwenye ndoa aliyoikusudia bali ni ndoa ndoana.Ni nani aliyempigia simu Husna? Alitaka nini? Lengo lake hasa ni nini? Ni kweli alichokusudia mpiga simu ndicho alichokihitaji ili kuvuruga ndoa hiyo? Nenda hatua moja moja kwa kusoma kila nakala ya toleo la Nipashe ili upate ukweli mzima wa kisa hiki cha utata, kusisimua, kusikitisha na chenye mafunzo makubwa kwa jamii na wanandoa wote.

# Simu ya Sumu-3

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

HIVI dada unajifanya umeolewa ee! Wewe ni mlinda nyumba tu. Mimi mwenzako hata ndugu zake wananifahamu hadi leo hii. Mimi ndiyo wanonitambua kuwa wifi yao na shemeji yao, wewe umekaa hapo kama boya tu." Haya ndiyo maneno yaliyoandikwa kwenye hiyo meseji.

Alitaka kupotezea, lakini donge lilimkaa rohoni hata mate yalishindwa kupita. Akaona hapana. Majira ya mchana, akiwa na dera lake lililochakaa na kupauka ambalo mara nyingi hushindia nalo tu nyumbani, akavaa kandambili ambazo huenda nazo bafuni. Hakuwa na haja ya kupata walau mafuta au kuweka nywele vizuri. Khanga moja alijifunga kiunoni, moja akiishika mkononi pamoja na mtandio wake ambao hata hakujisumbua kuuweka kichwani, badala yake akatundika begani. Huyo akaanza kukata mitaa kuelekea anakoelekea. Njiani alionekana kama chizi. Kila aliyemuona alishangaa. Alionekana anaongea peke yake. "Ameshavurugwa." Baadhi ya watu waliambizana njiani.

"Kumbe wanalijua hili, watanitambua." Mabibo na Manzese Tip Top sio mbali sana. Huko ndiko ukweni kwa Husna.

Wakwe halisi baba na mama Dan wote walishafariki kabla hata hajaolewa. Waliobaki ni wifi na shemeji zake tu ambao walikuwa wanaishi kwenye nyumba ya urithi wa wazazi wao.

Alifika Tip Top kwa kudra za Mwenyezi Mungu tu, kwani alipishana na watu, bodaboda, magari, mikokoteni, maguta wakati mwingine yeye mwenyewe akiwa hajui hata anapishana na nini. Akili yake haikuwepo alipo. Alikuwa akifikiria mengi yaliyomfanya awe kama kichaa.

************************************


Aliwakuta mawifi zake, hakutaka kuingia ndani. Kwa jinsi walivyomuona walishtuka. Tunda na Halima hawakuamini macho yao walipomuona wifi yao yuko kwenye hali ile.

Mara moja walidhani huenda kuna jambo baya limemkuta kaka yao Dan na mkewe amekuja kuwapa taarifa. Hiyo iliwafanya hata midomo yao kuwa na ganzi na kutetemeka kwa woga.

Haikuwa kawaida. Kwa muda huu mfupi tu ambao wamekaa na wifi yao, hawajawahi kumuona yupo kwenye hali hiyo.

Moja kwa moja walijua kuwa kuna kitu kisicho cha kawaida, au jambo baya limemtokea kaka yao.

"Wifi imekuwaje?" Tunda alijikakamua kumuuliza huku akitetemeka kwa woga.




Ghafla machozi yalianza kumtoka Husna ambaye amekaa barazani. Wakati huo huo, Belo kaka yake Dan, ambaye naye aliishi hapo hapo alifika na kukuta hali hiyo.

Naye alishtuka. "Shemeji imekuwaje? Kuna nini huko?" Akauliza. Hapo hapo, akamfuata na kutaka kumnyanyua ili kama kuna chochote kibaya, kama ugonjwa, maafa, kifo basi akawataarifu ndani na si hapo barazani ambako watu wengi wanapita.

Shemeji akakataa kwa ishara, lakini akiendelea kumwaga machozi. Jinsi alivyokuja, alivyovaa, mwonekano wake na anavyolia, huku akikataa kuingia ndani wala kusema kilichomleta, iliwatisha zaidi.

"Hivi kumbe nyinyi mnajua kama kaka yenu ana mwanamke mwingine?" Akatoa sauti yake kwa mara ya kwanza. Na maneno ya alichoongea kilikuwa ni swali, badala ya kujibu alichoulizwa mwanzo na shemeji na wifi zake.

Ni swali lililowachanganya zaidi na kushindwa kujua wajibu vipi. Waliondolewa kwenye ile dhana ya mwanzo ambayo walidhani huenda kaka yao amepatwa na matatizo kwani wanakumbuka wiki mbili zilizopita ndugu yao aliwaaga anakwenda Zanzibar kikazi.

Shemeji Belo? Wifi zangu, hivi kumbe nyinyi ndugu mnajua kama kaka yenu ana mwanamke mwingine halafu hamniambii? Wote nyinyi mnakuja kwangu nawakaribisha kwa furaha, nawapikia chakula, tunacheka na kufurahi kumbe mnaning'ong'a kisogo? Mmenifanya mimi kama taahira. Nimewakosea nini mimi?"

Husna alikuwa akiongea kwa sauti kali iliyovutia majirani na wapita njia ambao walimiminika na wengine kusimama kusikiliza kinacholalamikiwa.

> "Hivi kumbe nyinyi mnajua kama kaka yenu ana mwanamke mwingine?" Akatoa sauti yake kwa mara ya kwanza. Na maneno ya alichoongea kilikuwa ni swali, badala ya kujibu alichoulizwa mwanzo na shemeji na wifi zake.

Belo na dada zake hawakuwa na la kufanya wala la kusema. Walibaki kimya. Walionekana kumshangaa na kuonekana hawakifahamu anachokiongea. Ilikuwa ngumu kwao kumjibu au kumbembeleza. Hawakujua ni nini kimetokea kati yake ya mumewe hadi yakafikia yote haya.

Kumbe nyinyi ndugu kuna vitu vimo ndani ya moyo wenu? Mmenifanya mimi kama taahira. Sasa kwa nini kaka yenu alikuja kuniona mimi? Alikuja kunioa ili anidhalilishe?

Ndoa ina miezi miwili tu, imeanza matatizo hivi? Tutafika kweli? Hili mlikuwa mnalijua, haiwezekani ndoa bado changa hivi halafu kuna mtu anajitokeza kutaka kuivunja ndoa yangu. Ina maana huyo mtu alikuwa naye muda mrefu kabla ya mimi? Sasa kwa nini kaja kunioa mimi kama si kunidhalilisha? Kwa nini hakumuoa huyo? Kwa nini wanaamua kunivunjia nyumba yangu mapema hivi? Kwa nini wameamua hivi? Mimi hata siamini. Sasa kwa nini mnaniita wifi na shemeji, wakati mna shemeji wifi wengine?"

Akazidi kulalama dada wa watu, akiendelea kulia, akiangaliwa na umati wa watu.

Belo alimsogelea shemeji yake na akamwambia "Samahani shemeji, najua una hasira, nakuomba urudi nyumbani, halafu mimi nitakuja kesho tutaongea, tuyamalize."

Belo aliona isingewezekana kwa namna yoyote ile kuanza kuulizana maswali ya, "wewe nani kamwambia", au "una ushahidi," ambayo yangeweza kuongeza chumvi kwenye kidonda. Alichoona ni hasira na uchungu uliomithilika wa shemeji yake aliyekuwa akiongea, na kulia kwa uchungu huku akitetemeka, hivyo hakuona busara yoyote ile ya kuongea, au kumuuliza chochote kile.

Husna naye ni kama vile alikuwa ametoa nyongo yote. Aliongea kila kitu ambacho alikuwa anataka kukisema. Akatapika kila kitu kilicho moyoni mwake. Akajiona hana tena cha kuongeza. Alipomaliza kuyabwaga yaliyompeleka, aliinuka na kuondoka, bila kuaga. Akaondoka kama alivyokuja. Alivyokuja hakusalimua mtu na alipondoka hakuaga mtu.

**************************************

"Mmemsikia lakini wifi yenu?" Belo akawatumbulia macho dada zake nusu saa ya baada ya Husna kuondoka na watu kusambaratika.

"Mimi sikumuelewa ujue?" Tunda akajibu.

"Ndiyo hujamuelewa, lakini kwa jinsi alivyoonekana na alichoongea ni kama kuna kitu kakigundua au kakiona."

"Kitu gani hicho kaka? Si ulikuwa unamsikia hapa akisema kaka Dan ana mwanamke mwingine?"

"Sio hivyo tu Tunda, kasema hata sisi tunajua kama Dan ana mwanamke mwingine. Na siyo kama kaja kuuliza, anachokuwa anakiongea ni kitu ambacho inaonekana ana uhakika nacho." Belo akawakazia macho dada zake.

"Kwa hiyo sisi ndiyo tunajua?" Akadakia Halima.

"Huwezi kujua, yule siyo mwendawazimu. Na mpaka kafikia hatua ile. Ukimsikiliza utagundua kuwa anakieleza kile ambacho anakielewa."

"Kwanza kanitisha mimi, nikajua kuna nini tena? Kaka kimemkuta nini huko Zenji, kumbe wivu."

"Tunda ee, tulia, mambo haya hayatuhusu, mambo ya mtu na mkewe watamalizana wenyewe, ukiingilia utaonekana mbea."

"Mbona na nyinyi kama mnanichanganya, mna kitu mnakijua?" Akauliza Belo.

"Mmmh, kaka na wewe, tujue nini, Dan alivyokuwa msiri yule, huku mwenyewe hatukumfahamu hadi alipotangaza ndoa."

"Nyinyi dada zangu mnadharau sana, angalia shemeji alivyokuja hapa, yaani kama mwendawazimu, nywele timtim, nguo haielewiki, hakuna mtu anayepagawa kiasi kile halafu awe amesikia tu, sio kushuhudia, inabidi kwanza niwasiliane na Dan kujua kama kuna ukweli wa hili."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# KUMBE GIGY MONEY ALIYATAKA MWENYEWE

KUMBE mdomo wa Gigy Money ndio umesababisha kugombana na baba mtoto wake Mo Jay, na kisha kupelekwa polisi.

Katika video iliyosambaa mtandaoni, alisikika Gigy Money, akimtolea maneno makali mzazi mwenzake huyo huku akimtuhumu mambo mbalimbali ambayo anadai kufanyiwa na Mo Jay.

Mwanamuziki huyo mwenye utata mwingi, alisikika akidai kutaka kumuingiza katika masuala ya kishirikina na kumfuatilia katika maisha yake.

# HERITAGE KUJA KIAFRIKA ZAIDI

MASHABIKI wa kundi la Morgan Heritage, watarajie kupata ladha tofauti katika Albam yao mpya ya "Homeland" ambayo itatambulishwa April 21, mwaka huu.

Katika album hiyo ambayo ina miondoko ya Afro Fusion, pia kutakuwa na wanamuziki mbalimbali wa Afrika, kama Rj the Dj pamoja na Eddy Kenzo, Jose Chameleon toka Uganda na Otile Brown wa Kenya.

Mbali na wasanii hao, pia wameshirikishwa wakali kama Shaggy, Youssou, Popcaan, Beenie Man, Shatta Wale, Busy Signal, Alpha Blondy, Made Kuti, Carleton, Ice Queen Cleo, Macky 2 na wengine tokea Carribean na Afrika.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MODRIC: SIFIKIRII KUONDOKA MADRID

Mshambuliaji huyo anaamini atakubaliana na mabosi wa timu hiyo ili...

**MADRID, HISPANIA**

LUKA Modric amethibitisha kujitolea kwake Real Madrid huku kukiwa na tetesi za kutakiwa na klabu ya Al Nassr ya Saudi Arabia.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 yuko katika msimu wa 11 hapo Santiago Bernabeu, ameshinda mataji 22, lakini mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Amekuwa akitajwa analengwa na Al Nassr, ambayo ilimsajili Cristiano Ronaldo Desemba, mwaka jana baada ya kuachiwa na Manchester United.

Lakini alipoulizwa kuhusu mustakabali wake akiwa na Timu ya Taifa ya Croatia hapo juzi, Modric aliweka wazi kipaumbele chake ni kukubaliana na Madrid.

"Mapenzi yangu yanajulikana, kubaki Real Madrid," alisema katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mechi dhidi ya Wales iliyochezwa jana. "Ninaamini na ninatumaini itatimia.

"Mengine yaliyosemwa ni mawazo na uvumi tu. Narudia jambo lile lile kwa mara ya mia moja: Natumai na ninaamini nitasalia Real Madrid."

Modric, ambaye hapo awali alisema anataka kuhisi kama anastahili mkataba mpya, pia alikanusha madai Madrid wamemtaka kustaafu kuichezea Croatia.

Kiungo huyo wa zamani wa Zagreb na Tottenham Hotpur jana alitarajiwa kuchezea Croatia mechi yake ya 163 dhidi ya Wales katika mechi yao ya kwanza ya kufuzu Euro 2024.

Akiwa amechagua kutostaafu kufuatia kichapo cha Croatia katika nusu fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Ufaransa, Modric atampita Drazen Ladic kama mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kuwahi kutokea nchini mwake.

"Sikujua hilo kabla ya mkutano na sijui kama ni nzuri au mbaya!" Modric alisema. "Ninajisikia vizuri nikiwa na timu ya taifa na nina furaha kuwa hapa. Najisikia furaha ninapokuwa hapa.

## KWA UFUPI

**NAGELSMANN KUMRITHI CONTE**
KLABU ya Tottenham Hotspur imemweka Kocha Mjerumani Julian Nagelsmann mwenye umri wa miaka 35, aliyefukuzwa kazi Bayern Munich - kama chaguo lao namba moja kuchukua nafasi ya Mtaliano, Antonio Conte (53), kama bosi wao mpya. ***(Football Insider)***

**NAGELSMANN AKARIBIA SPURS**
TOTTENHAM Hotspur inataka kufanya mazungumzo na Julian Nagelsmann, baada ya kuarifiwa awali kwamba bosi huyo wa zamani wa RB Leipzig ana 'mapenzi' kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England. ***(Mail)***

**BARRY KUMFUATA TUCHEL**
THOMAS Tuchel mwenye umri wa miaka 49, atambeba kocha msaidizi wa Chelsea, Anthony Barry (36), kwenda kumsaidia majukumu huko Bayern Munich baada ya kuchukua nafasi ya Mjerumani, Julian Nagelsmann. ***(Telegraph)***

**BAYERN MUNICH ILIHARAKISHA**
KLABU ya Bayern Munich ilifanya haraka kumteua, Thomas Tuchel, kutokana na hofu huenda akafuatwa na Real Madrid au Tottenham Hotspur. ***(Mirror)***

**TUCHEL AMTAKA MENDY**
THOMAS Tuchel atajaribu kumsajili golikipa wa Senegal, Edouard Mendy, mwenye umri wa miaka 31 na kiungo wa kati wa Croatia, Mateo Kovacic (28), kutoka klabu yake ya zamani ya Chelsea. ***(Calciomercato, via Football.London)***

**KOVACIC AIBUKIA UNITED**
KLABU ya Manchester United imeungana na Manchester City na Liverpool katika mbio za kuwania huduma ya nyota, Mateo Kovacic mwenye umri wa miaka 28 kutoka Chelsea. ***(90Min)***

**BARCA YAMFUATA GUNDOGAN**
BARCERLONA imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester City na Ujerumani, Ilkay Gundogan, mwenye umri wa miaka 32, na wale wanaohusika katika mazungumzo kuhusu mustakabali wake wanaamini huenda akahamia Hispania. ***(Athletic)***

**PEPE KUIGHARIMU ARSENAL**
ARSENAL itamuuza mchezaji wao aliyeweka rekodi ya uhamisho, Nicolas Pepe, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Nice, huu lakini huenda ikawalazimu kumlipa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 27 ili kuondoka. ***(Sun)***

**PAQUETA KUONDOKA**
KIUNGO wa kati wa kimataifa wa Brazil na West Ham, Lucas Paqueta, mwenye umri wa miaka 25 ataondoka msimu wa joto ikiwa timu hiyo itashuka daraja. ***(Football Insider)***

**PSV KUMUUZA SANGARE**
KLABU ya PSV Eindhoven iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ivory Coast, Ibrahim Sangare, mwenye umri wa miaka 25, huku Arsenal, Chelsea, Liverpool na Tottenham zikionyesha nia ya kumtaka. ***(90Min)***

**CHELSEA KUCHANGISHA FEDHA**
MMILIKI wa Chelsea, Todd Boehly, amekubali kwa muda kuandaa mechi ya nyota wote ya kuchangisha fedha itakayochezwa kwenye Uwanja wa Stamford Bridge ifikapo Agosti, mwaka huu kwa ushirikiano na Shirika la kutoa misaada la Football for Ukraine. ***(Evening Standard)***

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
LUXEMBOURG
VERSUS
PORTUGAL
1 | 14.01
X | 6.25
2 | 1.21

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# MESSI, MBAPPE KUBAKISHWA PSG

**PARIS, Ufaransa**

RAIS wa Paris Saint-Germain, Nasser Al-Khelaifi, ana nia ya kuwabakisha Lionel Messi, Kylian Mbappe na Sergio Ramos katika klabu hiyo.

Kuondolewa katika hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kumetia shaka mustakabali wa baadhi ya wachezaji muhimu wa PSG, pamoja na Kocha Mkuu, Christophe Galtier.

Messi na Ramos mkataba wao unamalizika mwishoni mwa msimu huu, huku kukiwa na ripoti mchezaji huyo anaweza kurejea Barcelona wakati Mbappe pia akihusishwa kutaka kuondoka licha ya kusaini mkataba mpya mwanzoni mwa msimu huu ambao utamfanya kubakia klabuni hapo hadi mwaka, 2025.

Licha ya kutokuwa na uhakika katika klabu hiyo, Al-Khelaifi ana matumaini PSG watawabakisha wachezaji wao bora, ingawa pia anataka kuona vipaji vya vijana zaidi vikianzishwa ndani ya timu.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wa Messi, Mbappe na Ramos Ijumaa iliyopita, Al-Khelaifi aliliambia gazeti la Marca: "Watu wanataka kujua kinachoendelea.

"Hatutafanya makosa yoyote. Nadhani ni muhimu sana kuzingatia msimu wetu sasa.

"Tunazingatia vipaji vya vijana. Tutaendelea kuwekeza katika klabu na katika mabadiliko ya siku zijazo ndani ya akademi."

PSG kuondolewa kwa mara ya pili mfululizo katika hatua ya 16 bora ina maana kusubiri kwao kwa muda mrefu kubeba taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa Ulaya kunaendelea, huku Mauricio Pochettino akipoteza kibarua chake mwishoni mwa msimu uliopita licha ya kuisaidia klabu hiyo kunyakua taji la Ligue 1.

# Ancelotti aitwa kuinoa Brazil

**LONDON, England**

CASEMIRO ndiye mchezaji wa hivi karibuni zaidi wa Brazil kumtaja kocha wake wa zamani wa Real, Madrid Carlo Ancelotti, kwa nafasi iliyo wazi ya kocha mkuu wa Selecao hao.

Brazil bado hawajatangaza mrithi wa Tite, ambaye muda wake wa miaka sita wa kuinoa ulifikia kikomo baada ya mabingwa hao mara tano wa dunia kutolewa katika hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia la 2022 na Croatia.

Ramon Menezes, ambaye aliiongoza Brazil chini ya umri wa miaka 20 kutwaa ubingwa wa Amerika Kusini U-20 Februari, amechukua nafasi hiyo kwa muda katika mechi ya kirafiki dhidi ya Morocco uliyochezwa jana.

Hata hivyo, Ancelotti amekuwa kocha ambaye akihusishwa na jukumu hilo.

Wachezaji kadhaa wa Brazil wamesema waziwazi uwezekano wake na Casemiro alijiunga nao na aliwakumbusha wachezaji wenzake heshima la kuwaheshimu waajiri wa Ancelotti.

"Kwanza, kile ambacho sisi wachezaji tungependa kuwa nacho ni kocha mwenye uwezo na wachezaji wazuri,"alisema Casemiro akiwaambia waandishi wa habari Ijumaa.

"Kwa upande wa Ancelotti, ni kocha ambaye tayari namfahamu, namfahamu sana, ni rafiki yangu, ni mtu ambaye nimekuwa nikimkubali sana kwenye soka na ilikuwa ni furaha kufanya naye kazi.



HABARI MICHEZO

# YANGA : TUNATAKA KUMALIZA KWA HESHIMA MAKUNDI CAF

**Na Saada Akida**

BEKI wa Yanga Mkongomani, Djuma Shabaan, amesema wamejipanga kwenda kuweka heshima katika ardhi ya nyumbani kwao watakapowakabili TP Mazembe katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi kwenye mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

TP Mazembe itawakaribisha Yanga katika mechi ya michuano hiyo itakayochezwa Lubumbashi Aprili 2, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Djuma, alisema mechi hiyo itakuwa ngumu lakini neno ushindi limetawala katika vichwa vya wachezaji wote wa Yanga hasa kwa wale wenye uraia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Nyota huyo alisema ushindi dhidi ya TP Mazembe utawaheshimisha mastaa hao wanaocheza katika klabu hiyo ya Tanzania ambayo tayari wameshatinga hatua ya robo fainali.

"DRC ni nyumbani lakini nacheza Tanzania, ni maisha ya mpira na tuko hapa kuipambania Yanga ili ifikie malengo na kuweka heshima, hii mechi ya mwisho tunahitaji kuweka rekodi nzuri ya kuvuna pointi tatu nyingine dhidi ya TP Mazembe.

Ni timu kubwa Congo lakini na Yanga ni kubwa kwa Tanzania, sasa tunataka kushinda mechi hii ili kuonyesha ukubwa wa timu yetu katika michuano ya kimataifa," aliongeza beki huyo.

Wachezaji wengine wa Yanga ambao ni raia wa DRC ni Fiston Mayele, Yanick Bangala, Joyce Lomalisa na Jesus Moloko.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kibasila wakicheza mpira wa kikapu kwa ajili ya kukuza vipaji vyao kwenye Uwanja vya Jakaya Kikwete Youth Park ulioko, Dar es Salaam. **PICHA : JUMANNE JUMA**

# Stars yamkosha Rais Samia

INATOKA UK. 24

Aliongeza anaamini kujitoa kwa wachezaji na mashabiki, kutasaidia kufikia malengo ya timu hiyo.

"Mechi inayofuata tutacheza nyumbani, tunacheza tukiwa na mashabiki ambao ni mchezaji wa 12, mimi nataka kuona uwanja unajaa ili nifurahi na nitajiona ni mmoja wa makocha wakubwa Afrika," alisema kocha huyo.

Lilikuwa ni bao pekee katika mechi hiyo lililofungwa dakika ya 68 na Simon Msuva, nyota anayecheza soka la kulipwa katika kikosi cha Al-Qadsiah, Saudi Arabia.

Rais Samia pia anaendelea na ahadi yake ya kununua kila bao linalofungwa na Simba na Yanga katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika kwa Sh.milioni tano.

Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Shufaa Lyimo.


CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 26/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1655 | Numancia vs Real Murcia | 2.69 | 2.80 | 2.69 |
| 13:00 | 5869 | Merida UD vs Fuenlabrada | 2.12 | 2.95 | 3.46 |
| 13:30 | 2562 | Bodrumspor vs Erzurum BB | 1.71 | 3.49 | 4.21 |
| 13:40 | 3335 | Manchester City W vs Chelsea W | 2.75 | 3.27 | 2.32 |
| 14:45 | 2687 | Iraklis Larisas vs AE Larissa | 3.98 | 3.21 | 1.86 |
| 14:45 | 3023 | Niki Volou vs Makedonikos FC | 1.88 | 2.95 | 3.70 |
| 15:00 | 1603 | Zwickau vs Ingolstadt | 2.61 | 3.37 | 2.50 |
| 15:00 | 3217 | Forest Green vs Sheffield Wed | 6.86 | 4.14 | 1.44 |
| 15:00 | 4330 | Kolding IF vs FC Roskilde | 1.51 | 3.85 | 5.34 |
| 15:00 | 4472 | Eibar vs FC Andorra | 1.90 | 3.11 | 4.11 |
| 15:30 | 4390 | Catanzaro vs Pescara Calcio | 1.52 | 3.89 | 6.39 |
| 15:30 | 4903 | Willem II Tilburg vs Maastricht | 1.29 | 5.23 | 7.94 |
| 15:30 | 4948 | Calcio Lecco vs Triestina | 2.20 | 3.14 | 3.35 |
| 15:30 | 5082 | Heracles Almelo vs Den Bosch | 1.17 | 6.66 | 11.45 |
| 15:30 | 5532 | Telstar vs FC Oss | 1.73 | 3.64 | 4.16 |
| 15:30 | 5873 | Cesena vs Olbia Calcio | 1.72 | 3.42 | 5.12 |
| 16:00 | 1953 | Esbjerg vs BK Frem | 1.30 | 4.61 | 8.00 |
| 16:00 | 2435 | Sokol Brozany vs FC Kolin | 2.43 | 3.50 | 2.43 |
| 16:00 | 3108 | CA Fenix vs CA Boston River | 2.48 | 3.14 | 2.57 |
| 16:00 | 4894 | Kazakhstan vs Denmark | 10.22 | 5.22 | 1.32 |
| 17:00 | 2425 | Rayo Majadahonda vs Pontevedra | 2.10 | 3.10 | 3.31 |
| 17:15 | 4826 | Ponferradina vs Mirandes | 2.02 | 3.15 | 3.60 |
| 17:15 | 5913 | Zaragoza vs Albacete Balompie | 2.15 | 2.95 | 3.50 |
| 17:30 | 4502 | Solin vs Kustosija | 1.77 | 3.30 | 3.65 |
| 18:00 | 1575 | Russia vs Iraq | 1.54 | 3.97 | 6.22 |
| 18:00 | 1613 | Aduana Stars vs Real Tamale United | 1.27 | 4.44 | 11.36 |
| 18:00 | 1634 | CD Lagun Onak vs Leioa | 2.75 | 3.15 | 2.19 |
| 18:00 | 2042 | Terrassa FC vs UD Alzira | 1.93 | 3.14 | 3.65 |
| 18:00 | 5910 | Rudes Zagreb vs Orijent Rijeka | 1.43 | 3.85 | 5.60 |
| 18:15 | 2524 | Raith Rovers vs Hamilton | 2.12 | 3.31 | 3.06 |
| 18:30 | 1294 | Virtus Francavilla vs Monopoli | 2.77 | 3.09 | 2.60 |
| 18:30 | 2065 | Piacenza Calcio vs Novara | 3.34 | 3.02 | 2.27 |
| 18:30 | 4598 | Vicenza vs Arzignanochiampo | 1.59 | 3.74 | 5.76 |
| 19:00 | 1305 | Cornella vs Real Union Irun | 2.05 | 2.90 | 3.73 |
| 19:00 | 1860 | England vs Ukraine | 1.33 | 5.12 | 9.80 |
| 19:00 | 3447 | Eyupspor vs Caykur Rizespor | 1.79 | 3.39 | 3.91 |
| 19:00 | 3561 | Liechtenstein vs Iceland | 18.50 | 6.53 | 1.19 |
| 19:00 | 3601 | Slovenia vs San Marino | 1.10 | 9.35 | 32.62 |
| 19:00 | 4413 | San Sebastian Reyes vs Leonesa | 3.20 | 3.00 | 2.20 |
| 19:30 | 2939 | Villarreal B vs Huesca | 2.31 | 3.04 | 3.04 |
| 19:30 | 5319 | Granada vs Real Oviedo | 1.78 | 3.16 | 4.71 |
| 21:00 | 3351 | Atletico Grau vs Alianza Lima | 3.34 | 3.24 | 1.99 |
| 21:45 | 1188 | Malta vs Italy | 18.40 | 7.14 | 1.17 |
| 21:45 | 1375 | Northern Ireland vs Finland | 2.52 | 3.14 | 2.98 |
| 21:45 | 3330 | Luxembourg vs Portugal | 14.01 | 6.25 | 1.21 |
| 21:45 | 4642 | Slovakia vs Bosnia and Herzegovina | 2.55 | 3.21 | 2.89 |
| 22:00 | 1687 | Las Palmas UD vs Sporting Gijon | 1.70 | 3.35 | 4.90 |
| 23:00 | 2271 | Real Cartagena vs Barranquilla FC | 1.49 | 3.89 | 5.80 |
| 23:00 | 2545 | Real Santander vs Cucuta Deportivo | 2.28 | 2.95 | 3.11 |
| 23:30 | 3039 | Asociacion Deportiva Tarma vs FBC Melgar | 2.56 | 3.03 | 2.57 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Machi 26, 2023

Nipashe



**Modric: Sifikirii kuondoka Madrid**

UKURASA 21

# TAIFA STARS YAMKOSHA RAIS SAMIA

## ●●● Aahidi kununua goli kwa Sh. milioni 10, kocha aita mashabiki kwa Mkapa ili...

**Na Waandishi Wetu**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefurahishwa na ushindi walioupata Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Afrika (AFCON) dhidi ya Uganda (The Cranes), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Suez Canal mjini Ismailia, Misri juzi.

Ushindi wa bao 1-0 umeifanya Taifa Stars kufikisha pointi nne na kukwea hadi nafasi ya pili kwenye msimamo wa Kundi F ambalo linaongozwa na Algeria yenye pointi tisa.

Timu hizo zitarudiana keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wakati mechi nyingine ya kundi hilo itakuwa ni kati ya Benin dhidi ya Algeria.

Rais Samia amewapongeza wachezaji wote wa Taifa Stars, benchi la ufundi, viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na wadau wote ambao walishiriki katika maandalizi ya mchezo huo.

Mbali na furaha yake hiyo, Rais ameahidi kutoa kiasi cha Sh.milioni 10 kwa kila goli la Stars watakalofunga kuanzia mechi zinazofuata.

Salamu hizo za Rais Samia zimetolewa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, muda mfupi baada ya mechi hiyo ya Stars na Uganda kumalizika.

"Hongera sana Taifa Stars, hongera sana wachezaji, kwa kweli leo (juzi), mmetutoa kimasomaso Watanzania kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Uganda (The Cranes) na kwa kweli kila mmoja amefurahi sana, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amefurahishwa sana na ushindi huu katika mchezo uliofanyika nchini Misri, na kutokana na ushindi huo, mheshimiwa anawapongeza wachezaji wote wa Taifa Stars, benchi la ufundi, TFF na wadau wote ambao wameshiriki kwenye maandalizi.

Lakini zaidi ya hapo anataka Stars tufanye zaidi kwenye mechi yetu ya marudiano itakayofanyika tarehe 28, mwezi huu wa tatu hapa Dar es Salaam. Na katika kuwatia ari wachezaji ili kuwahamasisha, ameamua kutoa donge nono la Sh. milioni 10 kwa kila goli ambalo Stars watalifunga kuanzia mechi zinazofuata, yaani inayofuata na kuendelea hadi tutakapofuzu kwenda kucheza fainali za AFCON, michuano hii mikubwa kabisa barani Afrika," alisema Msigwa kwa niaba ya Rais Samia.

Msigwa alisema ushindi huo umeijengea heshima nchi na kuitangaza vizuri ndani na nje ya mipaka ya Tanzania, Afrika na dunia kwa ujumla.

"Hongereni Stars, na Watanzania wote, na kila la kheri," Msigwa aliongeza.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Adel Amrouche, amesema anawapongeza wachezaji kwa kufuata maelekezo yake na kusisitiza yeye huwa anaamini kwenye kushinda na si kushindwa.

Amrouche amesema siku zote amekuwa akiandaa timu kushinda na si kutoka sare au kupoteza.

"Nimejaribu kuita wachezaji wapya na wengine wazoefu, nimebadilisha falsafa ya timu, nia ni kubadili mitazamo, nadhani mashabiki wengi hawakuamini, lakini siku zote mpira unachezwa uwanjani," alisema Amrouche.

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva. **PICHA: TFF**

## Robertinho afunga hesabu kuivaa Raja

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' amesema mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca ambayo itachezwa ugenini haimzui kuweka mikakati ya michezo ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Raja Casablanca itaikaribisha Simba katika mechi ya mwisho ya hatua ya makundi itakayochezwa Aprili Mosi, mwaka huu nchini Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jana, Robertinho, alisema mchezo huo mmoja wa kukamilisha ratiba utakuwa mgumu na wamejipanga kupambana kupata matokeo chanya.

Robertinho alisema mbali na kuhitaji kumaliza makundi kwa heshima, tayari ameanza maandalizi mechi ya hatua inayofuata.

Alisema wako tayari kukutana na timu yoyote kwenye hatua hiyo na anaamini wataendelea kuweka rekodi msimu huu.

"Hizi mechi za hatua ya robo tutabadilika kidogo, unajua kama tutaanzia nyumbani halafu kwenda ugenini, tunatakiwa kumaliza kazi hapa halafu utajua ucheze vipi kule ugenini, kwa hiyo kifupi tutakuja na kitu kipya kingine," alisema na aliongeza;

Nilisema awali Simba haina sababu ya kuhofia mpinzani yoyote, mimi ni kocha ambaye napenda presha ya mechi kubwa kama hizi, hatukushinda dhidi ya Horoya kwa kubahatisha tulikaa na kuwasoma wapinzani wetu na kuwabadilishia mbinu zetu tofauti na tulivyocheza kwao," alisema kocha huyo.

Aliongeza amepanga mikakati sahihi katika hatua hiyo, kulingana na timu watakayopangiwa.

Wakati huo huo beki wa Simba, Mohammed Ouattara, amerejea kwenye uwanja wa mazoezi akiwa chini ya uangalizi mkubwa kabla ya kuanza programu ya kucheza na mpira.

Daktari wa Simba, Edwin Kagabo, alisema Ouattara amerejea mazoezini baada ya kukaa nje ya uwanja takribani wiki moja akiuguza majeraha.

"Ataendelea kufanya mazoezi chini ya uangalia kwa siku tatu kabla ya kuruhusiwa kujiunga moja kwa moja na wenzake, leo (jana) ameanza mazoezi mepesi na baada ya siku tatu ataruhusiwa kujiunga na wenzake," alisema Kagabo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >